Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA TATU

**Kikao cha Nane - Tarehe 6 Aprili, 2006**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Kabla hatujaingia kwenye shughuli za leo asubuhi nakuombeni Waheshimiwa Wabunge tuwatambue Waheshimiwa Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu wakiongozwa na Mwenyekiti wao wa Halmashauri hiyo. Ni wale wamesimama pale. Ahsante sana. *(Makofi)*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:**

Taarifa ya mwaka na Hesabu zilizokaguliwa za Serikali za Mitaa kwa kipindi cha mwaka kinachoishia tarehe 30 Juni, 2005 *(The Annual Report and Audited Accounts of the Local Authorities for the year ended 30th June, 2005)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):**

*The Statutory Report of the Controller and Auditor General on the Audit of the Financial Statements of Ministries Independent Departments and Affiliated Bodies for the Financial year ended 30th June, 2005.*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 105

### Madawa ya Kulevya

**MHE. PETER J. SERUKAMBA (k.n.y. MHE. ANNE K. MALECELA)** aliuliza:-

Kwa kuwa tatizo la vijana na baadhi ya watu wazima kutumia dawa za kulevya katika nchi yetu sasa hivi limekuwa kubwa sana na kwa kuwa dawa hizo zimekuwa ni chanzo kikuu cha kuathiri akili za watumiaji:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukomesha biashara hii haramu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, MAAFA NA KAMPENI DHIDI YA UKIMWI (MHE. DR. LUKA J. SIYAME)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Same Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwepo kwa tatizo la baadhi ya vijana na watu wazima kutumia dawa za kulevya hapa nchini na kwamba baadhi yao wameathirika kutokana na matumizi ya dawa hizo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kudhihirika kuenea kwa kasi kwa matumizi na biashara ya dawa za kulevya hapa nchini, mwaka 1991 Serikali iliamua kuanzisha Kitengo chini ya Jeshi la Polisi ili kukabiliana na tatizo hilo. Kadri muda ulivyokwenda, tatizo liliendelea kukua na hivyo kuhitajika mpango na mikakati zaidi ya kudhibiti matumizi pamoja na biashara ya dawa za kulevya. Mpango kabambe uliandaliwa na mikakati yake inatekelezwa kupitia Vitengo vilivyoanzishwa katika Jeshi la Polisi, Idara ya Ushuru wa Forodha na ndani ya Idara ya Usalama wa Taifa. Kwa pamoja vyombo hivyo vya Ulinzi na Usalama vimesaidia kudhibiti uingizaji na uzalishaji haramu wa dawa za kulevya hapa nchini. Mkakati mwingine unaotekelezwa ni wa uimarishaji wa ulinzi kwa kutumia vifaa vya kisasa katika viwanja vya ndege vya Kimataifa, bandari na mipaka ya nchi kavu.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hatua hizo, Serikali pia iliwasilisha Bungeni Muswada ambao ulipitishwa kuwa Sheria Na. 9 ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya ya mwaka 1995 kwa lengo la kupiga marufuku shughuli yoyote inayohusiana na suala la dawa za kulevya, isipokuwa kama dawa hizo zinahitaji kwa ajili ya matumizi halali na baada ya kupatikana kibali cha kuruhusu dawa hizo zitumike. Serikali kwa mujibu wa sheria hiyo, imeanzisha Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Tume hii inajumuisha Wajumbe ambao ni Mawaziri kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, vile vile Bunge hili Tukufu lilipitisha Sheria Na. 1 ya Chakula, Dawa na Vipodozi ya mwaka 2003 na Sheria Na. 3 ya Udhibiti wa Kemikali ya mwaka 2003 zote hizo zikiwa zinajenga na kuimarisha utekelezaji wa mikakati ya mpango huu. Aidha, marekebisho yote yaliyofanywa kwenye Sheria ya Uhamiaji, Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai na Sheria ya Udhibiti wa Mapato, yatokanayo na

uhalifu huo yote yalilenga kuwezesha utekelezaji wa mpango kabambe na Sheria Mama ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya.

Mheshimiwa Spika, kielelezo tosha juu ya juhudi za Serikali kuhusiana na dawa za kulevya ni kama nilivyoeleza katika jibu la swali Na. 38 nililolijibu hapa Bungeni tarehe 28 Machi, 2006 yaani kati ya mwaka 2000 na 2004, watu waliotuhumiwa kujihusisha na dawa za kulevya ni 27,555 na jumla ya kesi 20,514 zilifunguliwa Mahakamani kuhusiana na ama biashara, matumizi au kulima mazao ambayo ni jamii ya dawa za kulevya.

Mheshimiwa Spika, pamoja na utekelezaji wa mikakati hiyo, rai yangu kwa wananchi wote ni kuwa tusiiachie Serikali na vyombo vyake tu kukomesha biashara hii haramu, kila mmoja wetu anayo nafasi yake. Familia zina wajibu wa kuwaelimisha vijana juu ya athari za dawa za kulevya. Aidha, tushiriki kikamilifu bila woga kuwafichua wote wanaojihusisha na biashara hiyo ili hatua za kisheria ziweze kuchukuliwa dhidi yao na kuiwezesha nchi yetu kutokomeza kabisa biashara hiyo haramu. *(Makofi)*

**MHE. JOHN S. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, napenda kwanza kukushukuru kwa kuniona na kunipa nafasi hii.

Kwa kuwa suala la madawa ya kulevya ni jambo ambalo ni la kutisha ulimwengu wote na Serikali zote ulimwenguni linalishughulikia jambo hili kwa nguvu sana na hapa Tanzania kumetokea matukio mawili makubwa. Yapo mengine mengi lakini mimi ningependa nichukue haya mawili makubwa. Kwanza la Akasha ambaye alishikwa na madawa yenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 4 na la pili ni la kile kiwanda kilichoshikwa kule *Mbezi Beach.* Sasa ningependa kujua Serikali imefikia wapi na kama hivi vitu viko Mahakamani basi tujue Mahakama zimeamua nini kwa sababu kesi zote hizi zina zaidi ya miaka minne sasa?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, kesi ile ya Munisi hukumu ilishatolewa na alionekana na hatia na nasikia anaomba rufaa kwenda Mahakama ya Rufaa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu naomba urudie kwa taratibu.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, kesi ile ya *Mbezi Beach* ambayo ilikuwa inahusu mshitakiwa Munisi na wenzake ilishakwisha Mahakama Kuu. Alionekana na hatia na alihukumiwa kifungo kwa kweli siwezi kukumbuka ni miaka mingapi sasa hivi. Lakini alifungwa na anaomba rufaa kwenda Mahakama ya Rufaa.

Juu ya kesi ya Akasha ilishakwisha siku nyingi.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa vijana wengi wa Kitanzania wameathirika sasa na madawa ya kulevya. Je, Serikali haioni kuna

umuhimu wa kuwa na vituo maalum vya kuwakusanya vijana hao ili tuweze kuwasaidia waweze kurudia hali yao ya kawaida?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, MAAFA NA KAMPENI DHIDI YA UKIMWI (MHE. DR. LUKA J. SIYAME):** Mheshimiwa Spika, katika jibu la swali namba 38 la tarehe 30 Machi, 2006 nilijibu kwamba kuna vituo ambavyo vinashughulika na wale vijana kwenye ile hali tunayoita *acute faith.* Baada ya hapo hawa vijana ama wanakwenda kwenye vile vituo ambavyo tunaita vituo vya *rehabilitation* kwa kuweza kufanya wajaribu kurudia maisha ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, wengi wao wanashauri kwamba warudie kwenye familia zao ili waweze kuishi maisha ya kawaida kama raia wengine. Ndio hapo awali nimesisitiza kwamba tunaomba familia ziendelee kuwaelimisha hawa vijana juu ya athari za madawa ya kulevya. Katika hali hiyo tunaona kwamba vituo maalum vya kuwaweka hawa vijana *permanently* sawa sawa na jela kwa hiyo havifai. Tunachohitaji ni kuwarudisha hawa vijana maisha ya kawaida ya kijamii kwa kuwafunza ili waweze kuona ubaya wa matumizi haya.

Na. 106

**Mmiliki wa Shule ya Msingi Mlimani**

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO** aliuliza:-

Kwa kuwa nia ya mpango wa *MMEM* ni kuongeza idadi ya wanafunzi katika shule zote za msingi za Serikali; na kwa kuwa utafiti umeonyesha kuwa idadi ya wanafunzi katika Shule ya Msingi Mlimani inazidi kupungua kutokana na matatizo mbalimbali lakini kubwa likiwa ni kukosekana kwa mmiliki wa shule hiyo:-

(a) Je, Serikali inalifahamu tatizo hilo?

(b) Kama Serikali inalifahamu, je, ni juhudi gani zimefanywa ili wanafunzi wapatiwe huduma wanazostahili ikiwa ni pamoja na upanuzi wa majengo?

(c) Kwa kuwa ardhi, kimsingi ni mali ya Serikali na kwa kuwa Chuo Kikuu na Manispaa ya Kinondoni vipo chini ya Serikali, je, ni lini Serikali itatoa tamko rasmi la nani ni mmiliki halali wa shule hiyo?

**NAIBU WAZIRI , OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Susan Lyimo, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa idadi ya wanafunzi katika Shule ya Msingi Mlimani iliyopo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam idadi ya wanafunzi inapungua. Shule ya Msingi Mlimani kwa sasa ina wanafunzi 1,818, walimu 56 na madarasa 14. Mwaka 2001 ilikuwa na wanafunzi 2,233. Idadi ya wanafunzi katika shule hii inapungua kwa sababu zifuatazo:-

(i) Shule kutosajili wanafunzi kutoka maeneo mbalimbali ambayo ni maeneo ya mbali ya shule ile.

(ii) Jitihada za kurudisha kiwango kinachotakiwa cha wastani wa wanafunzi 800 kwa kila Shule ya Msingi.

(iii) Wanafunzi wengi wa Chuo Kikuu sehemu ya Mlimani, walimu wengi au wafanyakazi wengi wa Chuo Kikuu wanawapeleka watoto wao kwenye shule za kulipia.

(iv) Maeneo mengi ya jirani kujenga shule nzuri na zenye hadhi.

(b) Mheshimiwa Spika, Shule ya Msingi Mlimani imekuwa ikipatiwa huduma mbalimbali kama zinavyotolewa kwa shule nyingine zozote za Halmashauri hapa nchini. Shule hiyo pia inafaidika na Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Shule za Msingi *(MMEM)*. Jumla ya shilingi 62,665,049.03 zimetolewa na mpango huo kwa kipindi cha Desemba, 2001 hadi Februari, 2006. Aidha, shule hiyo ina idadi ya walimu 56 na jumla ya madarasa 14. Kwa hiyo, shule hiyo haina tatizo la kupatiwa huduma za msingi.

(c) Mheshimiwa Spika, Shule za Msingi za Serikali nchini ni mali za Halmashauri husika. Shule zote zimeandikishwa na kusajiliwa kisheria na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na kila shule kupewa namba ya usajili. Aidha, Shule ya Msingi Mlimani imesajiliwa na kupewa Namba *BS 02243* tangu mwaka 1967. Shule hiyo ni mali ya Halmashauri ya Manispaa ya Wilaya ya Kinondoni. Kwa hiyo, napenda kutamka rasmi kwamba Shule hii ina mwenyewe na mmiliki halali ni Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa majibu ambayo siyo ya kuridhisha ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu shule hiyo kimsingi ina matatizo makubwa na mpaka sasa hivi mpango wa *MMEM* haupo kwa sababu hamna darasa hata moja ambalo limejengwa na kwa hivyo uongozi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam unadai kwamba ile shule imejengwa kwenye kiwanja chake. Kwa hiyo, nilikuwa naomba kupata maelezo ni kwa nini basi kama iko chini ya Halmashauri kwa nini mpaka leo halijajengwa darasa hata moja kwa mpango wa *MMEM?*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, Shule ya Msingi Mlimani ina matatizo, lakini tatizo la madarasa kwao halipo.

Kama nilivyosema ina madarasa yapatayo 14 ambayo yanakidhi mahitaji ya shule ile. *(Makofi)*

**MHE. SAID AMOUR ARFI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Pamoja na maelezo mazuri aliyoyatoa Mheshimiwa Naibu Waziri katika Ofisi ya Waziri Mkuu, nilikuwa napenda kufahamu kwamba Serikali ilitoa maelezo katika Bunge hili Tukufu kwamba Elimu ya Watu Wazima iliteremka kutoka asilimia 96 mpaka asilimia 71 kwa sababu ya wafadhili kujitoa na mpango mzuri wa *MMEM* na *MMES* unachangiwa na wafadhili. Je, pindi wafadhili watakapojitoa Serikali imejiandaa vipi kuhusu mpango huu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge naona swali hili kama ni jipya. Tutafaidika ukiliuliza upate majibu kamili kikao kijacho. *(Makofi)*

Na. 107

**Barabara ya Kibiti - Kikale**

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA** aliuliza:-

Kwa kuwa Rais wa Awamu ya Nne, Mheshimiwa Jakaya Kikwete katika kampeni za uchaguzi hapo tarehe 18 Novemba, 2005 aliwaahidi wananchi wa Kibiti kuwa Serikali itajenga barabara ya Kibiti - Kikale ili kupunguza adhabu kubwa ya usafiri wanayoipata wananchi wa vijiji ambavyo barabara hiyo hupita:-

(a) Je, ni lini ujenzi wa barabara hiyo utaanza ili kutekeleza ahadi ya Rais?

(b) Je, ujenzi unaotarajiwa utakuwa ni wa kiwango gani?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdul Marombwa, Mbunge wa Kibiti, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli wakati wa Kampeni za Uchaguzi Mkuu mwaka 2005, Mheshimiwa Rais alitoa ahadi kwamba Serikali itaboresha barabara ya Kibiti - Kikale. Barabara ya Kibiti - Ruaruke kilometa 28.0 ni sehemu ya barabara kubwa ya Kibiti - Ruaruke - Kikale - Mtunda yenye urefu wa kilometa 47. Barabara hii hufanyiwa matengenezo na Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara *(Road Funds)*. Aidha, ili kutimiza ahadi hiyo, Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji mwezi Novemba, 2005 imefanya tathmini ya matengenezo ya barabara hizo kwa kiwango cha changarawe. Gharama zimekisiwa kuwa shilingi 940,000,000.

(b) Mheshimiwa Spika, Halmashauri italiwasilisha suala hili katika vikao vyake vya maendeleo ili kuangalia jinsi ya kuweka katika vipaumbele vya Wilaya na kutafuta fedha kwa wafadhili na katika Mfuko wa Barabara. Hata hivyo ili kuhakikisha kuwa

barabara hiyo inapitika kila wakati, mwaka 2006/2007 Halmashauri imetenga jumla ya shilingi 12,500,000 kwa ajili ya matengenezo ya kawaida. Aidha, tangu mwaka 2004/2006 jumla ya kiasi cha shilingi 54,807,966 zimetumika katika matengenezo ya barabara ya Kibiti - Ruaruke - Kikale - Mtunda. Vile vile barabara ya Kibiti - Ruaruke pekee kwa mwaka 2005/2006 imetengewa shilingi 7,840,000 kwa ajili ya matengenezo ya kawaida ambapo kilometa10.20 zimetengenezwa na maeneo korofi ya kilometa 1.6 pia zimetengenezwa.

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nilikuwa na swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa ametangaza kuwa kuna maeneo korofi ambayo yametengenezwa kiasi ya kilometa 7 nilitaka nimwombe Mheshimiwa Waziri je, alikwenda na kuona maeneo hayo korofi kwa sababu hayo maeneo mpaka sasa hivi hakuna aliyetengeneza kwa kipindi cha mwaka jana na mwaka huu. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, sio rahisi kwa Waziri kutembelea kila barabara hapa nchini. Lakini kwa kuwa Halmashauri zinatupa taarifa zote za utendaji wa barabara zote nchini tumepata taarifa rasmi ambapo mainjinia wetu wamekwenda kutembelea sehemu hiyo na hayo matengenezo yamefanywa kwa kiasi fulani. Nimesema tatizo halijaisha ila Serikali itakuwa inatengeneza mara kwa mara kwa sababu inatambua tatizo la barabara hiyo.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kuwa Mheshimiwa Rais alifanya ziara nchi nzima wakati wa Kampeni yake na kwa kuwa alitoa ahadi mbalimbali, je, Serikali haioni umuhimu sasa wa kuandaa orodha ya ahadi hizo na kuwakabidhi Wabunge wote nchini kuliko kuuliza maswali madogo madogo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, Serikali kwa sasa hivi imeagiza Halmashauri zote, Mikoa yote kuorodhesha zile ahadi zote ambazo zilitolewa na Mheshimiwa Rais na zitapelekwa kwenye Wizara husika na Wizara husika zitapanga mkakati wa kuzitekeleza kwa awamu kuanzia mwaka huu mpaka mwaka 2010. *(Makofi)*

Na. 108

**Ujenzi wa Ofisi ya Makamu wa Rais Zanzibar**

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI** aliuliza:-

Kwa kuwa Jengo la Ofisi ya Makamu wa Rais limekusudiwa kujengwa huko Zanzibar kwenye Jimbo la Mwanakwerekwe, eneo ambalo awali liliwekwa uzio na kwa kuwa wakati wa kuweka uzio huo mazao ya wananchi yaliyokuwepo yaliharibiwa, ikiwa na pamoja na jengo lililokuwa maskani ya Chama cha Mapinduzi kubomolewa ili kupata nafasi ya ujenzi wa Ofisi hiyo lakini hawakulipwa gharama za mali iliyoharibiwa:-

(a) Je, uzio uliojengwa kwenye eneo hilo uligharimu fedha kiasi gani?

(b) Je, ni lini wenye konde walioharibiwa mazao yao watalipwa fidia pamoja na jengo la Chama cha Mapinduzi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Uzio uliojengwa kwenye eneo la Mwanakwerekwe uligharimu shilingi 125,146,633.89 kwa mchanganuo ufuatao:-

(i) Gharama za Mkandarasi shilingi 107,127,735.89 kwa *Certificate* mbalimbali.

(ii) Gharama za kuhamisha mtandao wa simu shilingi 1,824,721 ambazo zililipwa kwa *TTCL.*

(iii) Gharama za kuhamisha laini ya umeme shilingi 11,677,186 ambazo zililipwa kwa Shirika la Mafuta na Nguvu za Umeme Zanzibar.

(iv) *Consultancy Fee* shilingi 4,020,000 zilizolipwa kwa Mkurugenzi wa Majengo, Wizara ya Ujenzi.

(v) Gharama za Upimaji Viwanja shilingi 500,000 zilizolipwa kwa Mkurugenzi Idara ya Upimaji wa Mipango Miji Zanzibar.

(b) Eneo lililojengwa ukuta lilikuwa linamilikiwa na Benki Kuu ya Tanzania, Tawi la Zanzibar na baada ya ujenzi kutoendelea eneo hilo limerudishwa Benki Kuu ya Tanzania , Tawi la Zanzibar. Kama nilivyoeleza eneo hilo lilikuwa la Benki Kuu, Tawi la Zanzibar hivyo, ofisi haitarajii kulipa fidia kwa mtu yeyote au Taasisi yoyote.

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri sasa nataka kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Zanzibar kuna umuhimu mkubwa sana wa kuwepo Ofisi ya Makamu wa Rais na mpaka sasa Serikali ina kigugumizi. Je, Ofisi hiyo itaanza kujengwa lini na sehemu gani ya Zanzibar? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Spika, Serikali haina kigugumizi kuhusu ujenzi wa ofisi ya Makamu wa Rais Zanzibar. Nataka tu nimwarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari kuna fedha za ujenzi wa ofisi hiyo katika bajeti ya ofisi ya Makamu wa Rais mwaka huu. Aidha,eneo limeshapatikana sehemu ya Tunguu Zanzibar. Kinachosubiriwa ni Serikali ya Mapinduzi Zanzibar itoe hati ya kiwanja hicho ili ujenzi uanze mara moja.

Na. 109

**Mauaji ya Mwanafunzi - Jimbo la Mkoani**

**MHE. ALI KHAMIS SEIF** aliuliza:-

Kwa kuwa wakati wa uandikishaji wa wapiga kura katika Daftari la Kudumu Mkoa wa Kusini Pemba, Jimbo la Mkoani kituo cha Shule ya Ng'ombeni walitokea watu wenye silaha na kumuua mwanafunzi Juma Omar kwa risasi na kumjerujhi Ndugu Bakar Ali Bakar pamoja na Shaibu Abeid:-

(a) Je, watu hao walikuwa ni askari?

(b) Kama ndivyo, walikuwa ni wa kikosi gani?

(c) Je, mpaka sasa ni hatua gani za kisheria zimechukuliwa dhidi ya watu hao?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mbunge wa Mkoani, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika taarifa yake kuhusu uandikishaji wa wapiga kura katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura katika Mkoa wa Kusini Pemba, ilizungumzia kwa kina suala la mauaji ya mwanafunzi katika Jimbo la Mkoani. Taarifa hiyo ya Serikali ilitolewa tarehe 2 Desemba, 2004 na Mheshimiwa Waziri Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 8 Aprili, 2005 Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ilitoa kauli ya Mawaziri mbele ya Baraza la Wawakilishi ambayo ilisomwa na Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Waziri Kiongozi kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba na Utawala Bora. Kauli hiyo ilirejea taarifa iliyotolewa na Waziri Kiongozi. Taarifa zote hizo kwa pamoja zilielezea kwa kina kadhaa nzima iliyojitokeza tarehe 1 Desemba, 2004 katika kituo cha Ng'ombeni cha uandikishaji wa wapiga kura katika Daftari la Kudumu ambapo kulitokea vurumai iliyosababisha kifo cha marehemu Juma Omar Juma. Mungu amlaze mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi kwa niaba ya Mheshimwa Waziri wa Usalama wa Raia, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mbunge wa Mkoani, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kutokana na ushahidi wa awali wa kimazingira inaashiria kuwa Askari wa Vikosi vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambao ni *KMKM, JKU* na *KVZ* ndio wanaotuhumiwa kuhusika na kifo hicho. Askari hao wakiwa na silaha walikuwa wakilinda nje ya mita 200 toka kwenye kituo cha uandikishaji wa Daftari la Kudumu cha Ng'ombeni, Mkoani, Pemba.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa uchunguzi wa kina wa tukio hili bado unaendelea hivyo hakuna mtu yeyote aliyefikishwa Mahakamani kuhusiana na tukio hilo. Baada ya uchunguzi kukamilika hatua za kisheria zitachukuliwa kwa watakaobainika kuhusika na kifo hicho na wale waliosababisha kupoteza ushahidi watashughulikiwa kwa mujibu wa sheria za nchi.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Spika, pamoja na jibu zuri la Mheshimiwa Naibu Waziri naomba kumwuliza swali moja la nyongeza:-

Je, kwa sababu tendo hili limepita muda mrefu utendaji huu wa Jeshi la Polisi katika *speed* hii, haoni kuwa Jeshi la Polisi linatia aibu nchi yetu katika utendaji huu?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Mbunge swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, si kwamba Jeshi la Polisi linatia aibu, ni kwa sababu ya kutafuta haki ili tuwajue wahusika na tuwashughulikie kwa mujibu wa sheria na kwa sababu mazingira yenyewe yalikuwa na utata sana lazima ulipe muda mzuri lifanye uchunguzi vizuri wa kina ili haki itendeke. *(Makofi)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, kwa ruksa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa tukio kama hili lilitokea katika eneo la Piki ambapo inatuhumiwa askari mmoja wa Kikosi cha *JKU,* aliuawa na raia na kilichotokea ni kwamba vikosi vyote pamoja na Jeshi la Polisi walivamia eneo hilo na kuwakamata watu wengi na kuwaweka ndani.

Mheshimiwa Spika, kwa nini ikiwa pale ambapo askari alituhumiwa kuuawa raia wameteswa na kukamatwa na kuwekwa ndani kwa nini tendo kama hilo kwa kuwa vikosi vinajulikana watu waliokuwa kwenye zamu ya kazi kwa nini wasiweze kujua ni nani hasa aliyehusika na tukio hilo na kukamatwa?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, kwa ruksa yako naomba nimjibu Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mbunge wa Jimbo la Wawi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, si kwamba nia yetu ni kuchelewesha ama nia yetu kwenda kinyume na taratibu, lakini nia kubwa ya Serikali hapa ni kufanya uchunguzi utakaopelekea kwamba haki inatendeka. Mazingira ya suala hili ni tofauti kidogo na mazingira ya wakati wa uandikishaji wa wapiga kura.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na matatizo mengi, mambo mengi yalijitokeza kulikuwa na utaratibu wa kuwazuia watu wasiweze kujiandikisha, kulikuwa na baadhi ya wafuasi wa vyama waliokuwa wakifanya vurugu ya kuwapiga maafisa wa Serikali wakiwemo masheha, wasimamizi wa uchaguzi na wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni suala ambalo kidogo mazingira yake yanautata hata kifo chenyewe kilichotokea kina utata. Ni mwanafunzi aliyekuwa chini wa umri wa miaka 17 ambapo hatukutegemea kuwa angekuwepo katika maeneo yale, kwa sababu alikuwa haruhusiwi kujiandikisha kama mpiga kura. Kwa hiyo, mambo haya yana utata kidogo.

Na. 110

**Jeshi la Polisi**

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA (k.n.y. MHE. NURU AWADHI BAFADHIL)** aliuliza:-

Kwa kuwa hivi sasa Jeshi letu la Polisi linaonyesha *double standard* pale linapokemea wananchi kutokuchukua sheria mikononi mwao kwa kuwapiga na kuwaadhibu wahalifu kabla ya kosa lenyewe kuthibitishwa mahakamani:-

Je, kwa nini Polisi siku hizi wanatoa vipigo vikali kwa watu wanaowakamata kabla ya uthibitisho wa kosa lenyewe, hiyo ni sheria gani inayowaruhusu kufanya hivyo?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nuru Awadhi Bafadhili, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hakuna sheria inayoruhusu askri polisi kupiga wanaowakamata bali wanatakiwa kutimiza wajibu wao kwa kuzingatia misingi ya Sheria, Kanuni na Taratibu za Jeshi la Polisi. Askari wanahimizwa kuzingatia haki za msingi za watuhumiwa hata wanapokuwa chini ya ulinzi wa askari polisi. Kitendo cha kumpiga mtuhumiwa ni kosa chini ya kifungu namba 5 (18) cha *Police Force Service Regulations* na inapothibitika kwamba askari polisi ametenda kosa hili huchukuliwa hatua za kinidhamu na kupewa adhabu inavyostahili ikiwamo kufukuzwa kazi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo Wizara ya Usalama wa Raia itakuwa karibu zaidi na Jeshi la Polisi kuona kuwa askari wanatimiza wajibu wao kulingana na misingi ya sheria na kuhakikisha kuwa haki za binadamu zinalindwa. *(Makofi)*

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na namna alivyoelezea haoni kwamba kuna umuhimu zaidi wa kuwapatia askari polisi mafunzo zaidi ya sheria ili kuwakumbusha wajibu wao?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, kwa ruksa yako naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba upo umuhimu wa kutoa mafunzo na hivi sasa Serikali inaandaa utaratibu maalum wa kutoa mafunzo kwa Jeshi la Polisi na tunafikiria pia hata kuongeza muda wao wanapochukua kozi zao zile. Lakini hata hivyo tuna utaratibu maalum wa semina mbalimbali tunazozitoa kwa ajili ya kuona kwamba haki za binadamu zinalindwa.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniruhusu kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri ya kuonyesha nia kwamba Serikali ina nia ya kuzingatia sheria katika utendaji wa polisi ningependa kujua ni hatua gani zilichukuliwa kwa polisi waliompiga risasi marehemu Marwa Nyasinge, tarehe 20 Julai, 2005 katika mgodi wa Nyamongo? Kwa sababu wengine waliofanya uhalifu huo Mahenge walishachukuliwa hatua kwa hiyo, naomba kujua Serikali inampango gani na suala hilo? *(Makofi)*

Pia niipongeze Serikali kwa hatua ilizochukua juzi kwa mwanafunzi aliyeuawa ambaye anaitwa Joel Magige na hatua za Serikali kwa kweli zimetia moyo wananchi wa Tarime kwamba sasa Serikali ya awamu ya nne itazingatia haki na sheria. Je waliotenda kitendo cha kumuua mwanafunzi huyu wamachukuliwa hatua gani?

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ni dhahiri hili ni swali linaleta mambo mapya katika eneo tofauti, ila sehemu ya pili ya swali ambayo ni pongezi naomba hilo uijibu Mheshimiwa Naibu Waziri. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, kwa ruksa yako naomba nimjibu swali lake la nyongeza Mheshimiwa Chacha Wangwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nizipokee pongezi zake na tunamshukuru sana na tunamtakia kheri na wananchi wa Jimbo lake wamemsikia kwamba ni Mbunge ambaye anasaidia wananchi katika Jimbo lake, ahsante sana.

Na. 111

**Ukosefu wa Madkatari Bingwa - Singida**

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA** aliuliza:-

Kwa kuwa kwa muda mrefu sasa Hospitali ya Mkoa wa Singida haina Daktari Bingwa hata mmoja na kwa kuwa Madaktari waliokuwa wameazimwa toka Cuba walifanya kazi kwa muda wa miezi michache sana na baadaye kutoweka bila ya wananchi kuelezwa sababu za kuondoka kwao na kwa kuwa wananchi wanahusisha vifo vya akinamama na watoto wa Mkoa huo na kutokuwepo kwa Madaktari Bingwa hospitali:-

(a) Je, ni lini Serikali ya Awamu ya Nne itaupatia Mkoa wa Singida Madaktari Bingwa ili kuweza kuondoa kero hiyo kwa wananchi?

(b) Je, ni sababu gani zilizosababisha Madaktari Bingwa toka Cuba waondoke?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakiri kwamba Hospitali ya Mkoa wa Singida haina Daktari Bingwa hata mmoja. Uhaba wa Madaktari Bingwa hapa nchini umezikumbuka karibu Hospitali zote za Mikoa kutokana na idadi ndogo ya Madaktari ambao wamekuwa wakihitimu toka Chuo cha Madaktari cha Muhimbili. Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii imeongeza kwa kiwango kikubwa idadi ya Madaktari wanaogharamiwa mafunzo ya Uzamili katika vyuo vya Muhimbili na *KCMC*.

Mheshimiwa Spika, kwa hivi sasa kuna jumla ya Madaktari 121 wanagharamiwa mafunzo ya Uzamili na Wizara yangu. Kati ya hao 78 wanachukua mafunzo katika Chuo cha Udaktari Muhimbili na 43 katika Chuo cha *KCMC*. Wizara pia imewapelekea madaktari 22 kusomea ubingwa katika nchi za Kenya, Uganda, Afrika Kusini na China.

Mheshimiwa Spika, sasa noamba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mbunge wa Singida Kusini, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Wizara itawapangia kufanya kazi kwenye hospitali ya Mkoa wa Singida, Madaktari Bingwa ambao watakuwa wanahitimu kila mwaka. Hata hivyo ningependa kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba upungufu wa Madaktari Bingwa ni sehemu ndogo sana ya sababu za kuwa na idadi kubwa ya vifo vya akinamama.

Mheshimiwa Spika, vifo hivyo vinaweza kuzuilika kwa kuzingatia kanuni za afya kama vile kuhakikisha lishe ya kutosha kwa mama wajawazito na watoto, kuwakinga wasipate *malaria* kwa kuwapatia vyandarua vinavyotiwa dawa, kupata chanjo, kuwahi kuwapeleka haraka kwenye vituo vya huduma mara wanapoanza kuugua, kupimwa wakati wa ujauzito na kuzalia katika kituo cha afya au hospitali yenye wataalam.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kipindi ambacho nchi yetu imekuwa ikikabiliwa na uhaba wa madaktari bingwa, Serikali iliomba msaada wa madaktari toka nchini China, Cuba na Misri na kuwapanga kufanya kazi katika baadhi ya Hospitali za Rufaa na Mikao ikiwemo Singida.

Katika makubaliano ya Serikali ya Cuba na Tanzania, Tanzania ilikubali kugharamia yafuatayo, usafiri, nyumba na malazi, posho na gharama za watumishi watakaowahudumia kama wapishi, walinzi na dereva

Mheshimiwa Spika, mkoa wa Singida uliopokea Madaktari watatu toka Cuba mwezi Aprili, 2004 ilitarajiwa kwamba Mkoa kwa kufuatana makubaliano ungewapa Madaktari hao nyumba zenye hadhi, usafiri na kuwasaidia mahitaji madogo madogo ili waweze kufanya kazi zao vizuri. Mkoa wa Singida haukuwatimizia masuala hayo.

Hata hivyo, baada ya kiongozi wao wa Ubalozi wa Cuba na timu ya Wizara ya Afya kutambua mapungufu hayo walikubalina kwamba Madaktari hao wahamishiwe Mkoani Ruvuma ambao ulikuwa umekwishaandaa nyumba na mahitaji mengine muhimu kwa ajili ya wataalamu hao.

Mheshimiwa Spika, hizi ndizo sababu kuu zilizopelekea wataalam toka Cuba kushindwa kufanya kazi.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza, pamoja na majibu ambayo hayaridhishi sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri na kwa kuwa amekiri kwamba ni kwa muda mrefu Mkoa wa Singida hauna Daktari Bingwa hata mmoja na hizo jitihada ambazo Madaktari wamepelekwa kwenda kusoma nchi za nje, wananchi wa Singida wangetaka kujua ni lini hasa watapata Madaktari Bingwa kwa ajili ya shughuli hiyo na kama haipatikani basi sisi Wabunge wa Mkoa wa Singida turuhusiwe kuchukua hatua za kufikisha jambo hili hata kwa Mheshimiwa Rais kwa maana ya kwamba Wizara imeshindwa?

Pili hizo sababu ambazo zimefanya mpaka wale Madaktari waondoke ama nyumba ama usafiri ni matatizo ya viongozi. Lakini kukosekana kwa Madaktari hawa wanaoadhibiwa ni wananchi, je Mheshimiwa Waziri haoni kwamba ni vizuri kuwachukulia hatua viongozi waliosababisha hali hiyo badala ya kuwaadhibu wananchi kukosa Madaktari?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mohamed Missanga, kama ifuatavyo:-

Kwa vile ni kweli kwamba kuna uhaba wa Madaktari kama nilivyosema katika jibu langu la msingi ni kwamba iwapo Madaktari watakapokuwa wameshahitimu basi tutakuwa na utaratibu wa kuwapeleka Madaktari kwa sababu sasa Wizara imepewa nafasi ya kuajiri Madaktari moja kwa moja kutoka katika vyuo wanavyohitimu. Kwa hiyo, suala hili tutalizingatia.

Mheshimiwa Spika, katika swali lake la pili ni kweli kabisa kwamba lilikuwa ni suala la uongozi lakini ningependa kumwomba Mheshimiwa Mohamed Missanga, pamoja na Wabunge wenzake kwamba wale ambao walifanya tatizo hilo likasababisha kwamba wananchi wasipate huduma hizo basi Wizara itaangalia sababu ilikuwa ni nini iliyoletelezea hapo, lakini vile vile nashauri iwapo watakuwa wamekidhi matakwa yale kwa sababu bado tunategemea kupata Madaktari kutoka nchi hizi basi tutawapatia na tutaomba kushirikiana nao ahsante.

**MHE. ABDUKARIM E. HASSAN SHAH:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii kuuliza swali dogo la nyogeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika Bunge lililopita moja ya majibu yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya wakati ule Mheshimiwa Dr. Hussein Mwinyi, alisema Serikali ilikuwa ina mpango wa kupata Madaktari kutoka Cuba na Misri na moja ya Wilaya ambayo ilikuwa imeambiwa itapata huduma hiyo kutokana na upweke ilivyo ilikuwa ni Wilaya ya Mafia.

Je, mpango ule umeishia vipi na vipi Wilaya ya Mafia nayo itaweza kupata Madaktari hawa Bingwa kwa sababu sasa hivi tunapata miezi mitatu mara moja kwa *flying doctors* na hali ya akinamama haswa wajawazito wanakufa kila siku katika Wilaya ile baada ya kushindwa kupata Madaktari Bingwa kuja Tanzania Bara?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdulkarim Shan, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kuna Madaktari ambao wanakuja kutoka China na Misri. Hawa Madaktari ambao wametoka Cuba wao wanakuja kwa *contract* ya miaka miwili na kama nilivyosema walikuja mwaka 2004 kwa hiyo, *contract* yao inaisha mwaka 2006.

Mheshimiwa Spika, Wizara sasa hivi inatarajia kupokea Madaktari wengine sita kutoka Cuba na mara watakapofika basi tunaweza tukaangalia utaratibu wa kuwapeleka kule Mafia, lakini vile vile Madaktari ambao wametoka Misri sasa bado tunafanya utaratibu wa kuweza kuwapata na iwapo watapatikana tutaangalia utaratibu wa kuwapatia.

Na. 112

**Barabara zinazoingia Mlima Kilimanjaro**

**MHE. LUCY F. OWENYA** aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, kwenye *typing pool* hawaku-*type* maelezo yangu ya msingi ambayo yanahusu hifadhi ya Mlima Kilimanjaro ambayo hifadhi hii inaliingizia Taifa fedha nyingi za kigeni na pia ni mojawapo ya kivutio cha utalii nchini, baada ya maelezo hayo naomba sasa swali langu lifuatalo lipatiwe majibu.

(a) Je, Serikali inaelewa hali mbaya ya barabara zinazoelekea kwenye milango (*gates*) za Machame, Umbwe, Mweka na Londorosi hasa wakati wa kipindi cha mvua?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuzitengeneza barabara hizo ili ziweze kupitika kwa majira yote ya mwaka?

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka vyoo vyenye hadhi kwenye *camps* za njia zitumikazo na wapanda mlima huo?

**SPIKA:** Naomba radhi ni kweli swali kamili limekosewa kwa sababu maelezo ya utangulizi amekwisha yasoma natumaini Mheshimiwa Naibu Waziri swali kamili lilivyokuja Wizarani ni kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge. Unao ule utangulizi na kwa hiyo, unaweza kulijibu kikamilifu ahsante sana. Naomba radhi kwa niaba ya *typing pool.*

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lucy Owenya, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na ( c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inafanya jitihada kuhakikisha kuwa barabara zinazoingia Mlimani Kilimanjaro kwenye milango ya Machame, Umbwe, Mweka na Londorosi zinapitika wakati wote wa mwaka. Barabara zilizotajwa ziko chini ya usimamizi wa mamlaka za Halmashauri za Moshi Vijijini na Hai.

Mheshimiw Spika, lakini kutokana na umuhimu wa barabara hizo kwa shughuli za utalii, uhifadhi na kijamii. Hifadhi ya *KINAPA* imekuwa izifanyia matengenezo barabara hizo kwa nyakati tofauti kwa mfano:-

(a) Barabara ya Mweka kati ya mwaka 2003/2004 hadi Februari, 2006, jumla ya shilingi milioni 11,578,819 zilitumika.

(b) Barabara ya Machame kati ya mwaka 2003/2004 hadi Februari, 2006, jumla ya shilingi milioni 39,562,000 zilitumika.

(c) Barabara ya Londorosi mwaka 2003/2004 shilingi milioni 3,000,000 zilitumika.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kuwa barabara hizo zinapitika majira yote ya mwaka, *TANAPA* imenunua greda na kwa kushirikiana na Halmashauri husika imepanga kutengeneza barabara ya Mweka na Machame kwa kiwango cha lami kutegemeana na uwezo wa kifedha.

Mheshimiwa Spika, tatizo la vyoo katika milima mirefu ni tatizo la dunia nzima kama ilivyo kwa Mlima Kilimanjaro. Katika Ukanda wa juu ya milima hususan mita 3,000 juu ya usawa wa bahari na kuendelea, hali ya hewa huzuia kinyesi kisioze na

kulainishwa na *bacteria* kwa urahisi. Kwa muda mrefu *TANAPA* imekuwa ikitafuta aina ya choo inayofaa kwa mazingira ya Mlima Kilimanjaro. Ili kupata ufumbuzi wa tatizo hili, *TANAPA* imehusisha wataalam wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Ardhi na Usanifu wa Majengo katika kuchunguza na kufanya ubunifu wa vyoo muafaka. Baada ya kufanya utafiti, wataalam hao hatimaye wamefanikiwa kubuni aina ya choo kilichozingatiwa sifa zote muhimu zinazotakiwa na ambacho kitafaa. Taarifa za michoro na gharama zimekwisha wasilishwa *TANAPA*.

Mheshimiwa Spika, fedha za kujenga vyoo vitatu vya majaribio zimeombwa katika Bajeti ya mwaka 2006/2007. Iwapo vyoo hivyo vitathibitishwa kufaa kama inavyotarajiwa, jumla ya vyoo 70 vya aina hiyo vitajengwa katika kambi zote za Mlima. Wakati ujenzi huo unasubiriwa, *TANAPA* tayari imejenga vyoo vinne vyenye matundu 11 vyenye hadhi ya kuridhisha katika kituo cha Barafu na vingine viwili vyenye matundu manne vitajengwa kwenye kituo cha Shira II kabla ya mwisho wa mwezi Juni, 2006. Ni matumaini ya Serikali kuwa vyoo hivi vyenye hadhi vitaboresha sana huduma.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri na kwa kuwa Kilimanjaro ni mojawapo ya hifadhi ambayo inaingizia Taifa fedha nyingi za kigeni na zile barabara zinazoelekea Uhuru wakati ikitokea dharura si rahisi kwa gari za *KINAPA* kwenda kufanya *risk* kule juu.

Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kununua helkopta itumike kama *ambulance* ya mtu ambaye anapata ajali badala ya kukodisha helkopta nchi jirani?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, barabara zote, ambazo ziko kwenye hifadhi zote za Taifa, ikiwa na pamoja na hifadhi ya Mlima Kilimanjaro ni barabara nzuri na zinapitika kwa wakati wote. Kwa maana hiyo hakuna sababu ya kununua helkopta kwa wakati huu.

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri nilikuwa na swali moja tu dogo la nyongeza. Kwa kuwa moja barabara muhimu sana kwa utalii Mikoa ya Kusini ya Kyela -Matema jana usiku imesombwa kwa maji kama ambavyo inasombwa kila mwaka katika miaka 45 toka uhuru.

Je, Mheshimiwa Waziri anaweza tukakubaliana naye leo tukae chini na Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, tutatue hili tatizo dogo la kilometa moja tu ambayo inawasumbua watu na kukata kabisa utalii kwa miaka yote 45?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kama tunavyofahamu awamu ya nne inazingatia kufanya kazi na kuondoa matatizo ya wananchi kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya. Mimi na Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, mara baada ya kikao hiki tutakutana tuweze kuona jinsi gani tunaweza kuweza kutatua tatizo la barabara ya huko Kyela. *(Makofi)*

Na. 113

**Ujenzi wa Vyumba vya Madarasa Kondoa**

**MHE. PASCAL C. DEGERA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Utamaduni iliahidi kutoa fedha za *MMES* kwa ajili ya ujenzi wa vyumba kumi na sita vya madarasa katika Shule za Sekondari za Msakwalo, Farkwa na Sikwakwa katika Jimbo la Kondoa Kusini na kwa kuwa Serikali imetoa fedha kwa ajili ya vyumba sita tu.

(a) Je, Serikali haioni kuwa kutokutekeleza ahadi yake inawakatisha tamaa wananchi katika jitihada zao za kujiletea maendeleo?

(b) Je, ni kwa nini Serikali haikutekeleza ahadi hiyo?
(c) Je, Serikali sasa ina mpango gani wa kutekelezwa ahadi yake?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Pascal Degera, Mbunge wa Kondoa Kusini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari *(MMES)* 2004/2009 unatekelezwa na Wizara kwa kushirikiana na wananchi pamoja na washiriki wetu katika maendeleo *(development partners).* Aidha, mpango huu unaunga mkono juhudi za wananchi.

Katika utekelezaji wa *MMES* Serikali ilitarajia kupata shilingi bilioni 137.5. Hata hivyo, kiasi kilichopatikana ni shilingi bilioni 52.6 sawa na asilimia 38 tu, kufuatia hali hiyo, Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa ilipata ruzuku ya maendeleo kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madaraka 28 na nyumba 8 za walimu ambapo shule ya Sekondari Msakwalo ilipewa ruzuku kwa ajili ya ujenzi wa madarasa mawili na shule ya Farkwa ilipata ruzuku kwa ajili ya ujenzi wa madaraka mawili na nyumba moja ya mwalimu. Serikali haina nia ya kukatisha tamaa wananchi kwani inatambua na kuthamini mchango wao katika utekelezaji wa *MMES.* Kwa hiyo, itaendelea kutoa ruzuku ya maendeleo kwa ajili ya ujenzi kadri fedha zinavyopatikana.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuzipongeza Halmashauri zote na wananchi nchini kwa kuendelea kujenga shule za sekondari ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi wanaofaulu kuingia shule za sekondari. Aidha, Serikali itaendelea kushirikiana na wananchi kutimiza azma ya kuongeza asilimia ya wahitimu wa darasa la saba wanaojiunga na elimu ya sekondari. Naomba wananchi wasikate tamaa katika jitihada za kujiletea maendeleo kwa kuwa shule hizi zetu kwa ajili ya vijana au watoto wetu.

**MHE. PASCAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Aidha, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Kwa kuwa wananchi walihamasika sana na wakajenga maboma na sasa hivi kuna maboma kumi ya madarasa ambayo hayajaezekwa na kwa kuwa kipindi hiki ni kipindi cha njaa wala hawana uwezo wa kuweza kukamilisha na sasa wanafunzi wanasoma chini ya miti.

Je, Wizara haioni kuna haja ya kuwasaidia wananchi hawa ili watoto wao waweze kusoma katika mazingira mazuri kwa kuezeka yale madarasa kumi ambayo yamekwisha jengwa?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba wananchi walihamasishwa vya kutosha katika kujenga maboma hayo na kwamba ahadi ya Serikali ilikuwa ni kuwasaidia kumalizia na bado ahadi hiyo ipo, mara fedha zitakapopatikana ingawa hatuna hakika zitakuwa ni kiasi gani lakini kidogo kitakachopatikana kitagawanywa ili kuweza kuwasaidia wananchi katika ujenzi wa hizo shule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, kama itakumbukwa katika Bunge lililoahirishwa, Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa maelekezo namna gani Halmashauri zingeweza kusaidia kumaliza majengo hayo ili wanafunzi wapate mahali pa kusomea.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye swali la msingi kwamba tunazipongeza Halmashauri, kwa kweli zimesaidiana na zimetoa ushirikiano mkubwa na bado tunaendelea kuziomba na ndiyo maana tunazidi kuwasihi wananchi wasikate tamaa tuendelee kusaidiana kwa faida ya watoto wetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wanafunzi wanaosoma chini ya mti, suala hili tutalifanyia kazi ili tuweze kuona hawasomi chini ya mti na kwamba Halmashauri husika itabidi ifanye juhudi za ziada suala hilo lisiwepo. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ahadi hii ilitolewa na haijatekelezwa. Kwa mfano katika Mkoa wa Dodoma ilikuwa vyumba vya madarasa 16 katika Wilaya ya Kondoa, vyumba vichache zaidi ya hapo katika Wilaya ya Kongwa na vyumba vitano tu kwa Wilaya ya Mpwapwa. Kwa kuwa Waheshimiwa Wabunge tumelalamikia sana suala la mgao usiokuwa na uwiano wa mpango mzima huu wa *MMES,* je, Serikali itakubali kwamba fedha za utekelezaji wa mpango wa *MMES* zitakapopatikana sasa zitagawanywa kwa uwiano mzuri zaidi kuliko hali ilivyo sasa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba matarajio ya fedha kama nilivyoeleza kwenye jibu la msingi ilikuwa mpango mzima ugharimu

shilingi bilioni 137.5, lakini tulipata bilioni 52.6. Ni ukweli kwamba fedha hizo zilikuwa ni chache na kamwe zisingeweza kukidhi mahitaji yetu.

Mheshimiwa Spika, awali nilieleza kwamba kiasi kidogo cha fedha kitakachopatikana kwa kipindi chote hiki ambacho tunasubiri sasa hivi zitagawanywa ili madarasa yaweze kukamilika. Utaratibu itabidi uzingatiwe kwa kuangalia kipaumbele ni wapi kwa sababu fedha hiyo haitaweza kukidhi mahitaji yetu. *(Makofi)*

Na. 114

**Uhaba wa Walimu Wilaya ya Kahama**

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE** aliuliza: -

Kwa kuwa mpango wa *MMEM* unatenga fedha kuboresha Elimu ya Msingi kwa kuongeza vyumba vya madarasa na nyumba za walimu na kwa kuwa Wilaya ya Kahama na Mkoa wa Shinyanga zina uhaba mkubwa wa walimu ambapo wastani wa mwalimu kwa mwanafunzi ni 84.45 kwa sasa: -

(a) Je, Serikali ina mpango gani mahsusi kwa Wilaya ya Kahama kukabiliana na tatizo hili?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Chuo cha Ualimu Wilayani Kahama?

(c) Je, Serikali inafikiriaje kukipanua Chuo cha Ufundi Mpera ili kiwe kinafundisha taaluma ya ualimu sambamba na Chuo cha Ufundi?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ezekiel Maige, Mbunge wa Msalala, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, ili kupunguza tatizo la uhaba wa walimu katika Shule za Msingi, Serikali kupitia Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi *(MMEM)* huandaa na kuajiri Walimu katika Halmashauri zote nchini. Kuanzia mwaka 2002 hadi 2006 jumla ya walimu 50,546 wameajiriwa. Hii ni sawa na asilimia 110 ya lengo la kuajiri Walimu 45,796.

Hata hivyo, mahitaji ya walimu bado ni makubwa kwani wastani wa walimu kwa wanafunzi Kitaifa ni 1:55. Lengo ni kufikia wastani wa 1:40. Hii ni kutokana na ongezeko kubwa la uandikishaji wa wanafunzi. Kwa kipindi cha 2002 hadi 2005 Halmashauri ya Wilaya ya Kahama ilipangiwa jumla ya walimu 942 ambapo walimu 781 sawa na asilimia 83 waliripoti katika shule walizopangiwa. Mkoa wa Shinyanga kwa mwezi Machi, 2006 ulipangiwa jumla ya walimu 523, kati yao walimu 121 walipangiwa

Wilaya ya Kahama. Serikali itaendelea na juhudi za kuandaa na kuajiri Walimu wengi zaidi kadri inavyowezekana.

(b) Mheshimiwa Spika, vyuo vinavyoendesha mafunzo ya ualimu lengo lake ni kukidhi mahitaji ya walimu bora na wa kutosha katika Shule za Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu. Vyuo vya Ualimu ni vya Kitaifa, havigawanywi kimkoa wala Wilaya. Vipo Vyuo vya Ualimu 34 vya Serikali na vyuo 13 vya binafsi ambavyo hutoa mafunzo ya Walimu wa Daraja *A* na Stashahada. Vyuo vyote hivyo huchukua wanachuo wenye sifa kutoka Mikoa na Wilaya zote na wahitimu hupangwa katika Mikoa na Wilaya zote Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, kwa hivi sasa Serikali haina mpango wa kujenga Chuo cha Ualimu katika eneo lililotajwa na Mheshimiwa Mbunge.

(c) Mheshimiwa Spika, kuhusu Chuo cha Ufundi Mpera kutoa mafunzo ya ualimu sambamba na ufundi, Serikali haina mpango wa kutoa mafunzo ya ualimu katika Chuo cha Ufundi Mpera kwani chuo hicho kinahitaji kuimarishwa na kuongezewa nafasi ili kichukue vijana wengi wa mafunzo ya ufundi kwa lengo la kukidhi soko la ajira.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja dogo tu la nyongeza.

Kwa kuwa tatizo la Walimu Wilaya ya Kahama linasababishwa hasa na ugumu wa mazingira ya kikazi kwamba maeneo mengi hayana huduma muhimu kama barabara, maji na huduma za afya kwa hiyo walimu wengi wanapoajiriwa wanahama baada ya muda mfupi. Je, Wizara inafikiriaje kuweka mkakati maalum utakaosaidia kuwalipa posho walimu hao wanaofanya kazi kwenye mazingira magumu ili waweze kuvumilia kuishi kwenye maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA):** Mheshimiwa Spika, matatizo katika nchi yetu ni mengi ambayo yanasababisha walimu wengi wasiweze kwenda katika maeneo mengi, si katika Wilaya ya Kahama tu, yapo maeneo katika Mikoa ya Kigoma, Rukwa, Ruvuma, Mtwara, Lindi na hata Pwani. Matatizo haya ni pamoja na ukosefu wa nyumba za walimu, barabara, maji na mambo mengine kadha wa kadha. Matatizo haya ambayo yanasababisha walimu wasikae katika Mikoa au Wilaya kadhaa tunaweza kuyapunguza kwa Halmashauri kujipangia mipango thabiti ili kujenga nyumba za walimu na kuwapatia walimu mazingira mazuri ili waweze kukaa katika maeneo hayo. Ni ushauri wa Wizara ya Elimu, Wilaya na Halmashauri zijitahidi kupanga mipango ya kuhakikisha kwamba inaandaa mazingira mazuri kwa ajili ya walimu hasa wapya wale wanaokwenda kuripoti katika Halmashauri zao. *(Makofi)*

Suala la pili linalohusu barabara na maji, nalo pia ni suala ambalo Halmashauri zinapaswa kushiriki kuweza kuandaa ili walimu waweze kubaki katika Wilaya zao. *(Makofi)*

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuuliza swali moja la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, kwa kuwa Mkoa wa Shinyanga uko nyuma katika maendeleo ya sekta ya elimu, hali ambayo hivi karibuni ilimsikitisha Mheshimiwa Waziri Mkuu. Je, Serikali ina mpango gani wa dharura kuunusuru Mkoa wa Shinyanga kutoka katika hali iliyopo hivi sasa ili uweze kwenda sambamba na kasi mpya, nguvu mpya na ari mpya katika sekta ya elimu? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Ngoja nimsaidie mimi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi nizungumze machache zaidi ya yale majibu mazuri aliyotoa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa kumjibu Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli Waziri Mkuu alitembelea Mkoa wa Shinyanga, akaona matatizo ya Shinyanga. Naamini kabisa Mheshimiwa Mbunge anajua kwamba wiki ijayo nakwenda Shinyanga kufuatilia ziara ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa hiyo, ni kutokana na ziara hiyo ya kazi ambayo itatusaidia kujua vipi Serikali Kuu iingilie kati na vipi Halmashauri ichangie. Nashukuru sana. *(Makofi)*

Na. 115

**Kilimo cha Muhogo**

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED** aliuliza: -

Kwa kuwa zao la muhogo linalimwa sana Barani Afrika, Asia na *Latin America: -*

(a) Je, Tanzania ni nchi ya ngapi katika Bara la Afrika kwa uzalishaji wa muhogo na ni nchi gani duniani ni mnunuzi mkubwa wa zao hilo?

(b) Je, tani moja ya zao hilo inauzwa kwa kiasi gani cha fedha?

(c) Je, Tanzania inasafirisha tani ngapi kwa mwaka?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mbunge wa Wawi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, Tanzania ni nchi ya nne katika Bara la Afrika kwa uzalishaji wa zao la muhogo ambalo huzalisha wastani wa tani milioni 5.5 za muhogo

kwa mwaka. Nchi nyingine zinazozalisha zao la muhogo kwa wingi ni pamoja na Nigeria ambayo ni nchi ya kwanza kwa uzalishaji wa zao la muhogo duniani kwa kuzalisha wastani wa tani milioni 33 kwa mwaka, ikifuatiwa na Jamhuri ya Demokrasia ya Congo kwa kuzalisha wastani wa tani milioni 15 kwa mwaka na Ghana tani milioni 8.5 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, nchi za Jumuiya ya Ulaya *(European Union)* ndizo zinazoongoza kwa ununuzi wa muhogo ambapo hununua wastani wa tani milioni 7 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, katika Jumuiya hiyo, nchi ya Spain ndiyo mnunuaji mkubwa ambayo hununua wastani wa tani laki 8 kwa mwaka ikifuatiwa na Uholanzi tani laki 7.5 na Ubelgiji tani laki 6. Nchi nyingine ambazo hununua kiasi kikubwa cha muhogo ni pamoja na China ambayo hununua wastani wa tani milioni 2.5, Japan tani laki 7 na Marekani tani laki 1 kwa mwaka.

Hata hivyo, katika miaka ya 2000 sehemu kubwa ya muhogo unaosafirishwa kutoka Tanzania huuzwa katika nchi jirani za Burundi, Rwanda, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo na Kenya. Kwa mfano, katika mwaka 2005 jumla ya tani 814 zilisafirishwa kwenda nchi ya Rwanda. Nchi nyingine ya Mashariki ya Kati inayonunua zao la muhogo kwa kiwango kidogo ni nchi ya Falme za Kiarabu ambayo katika mwaka 2003 ilinunua kilo 300 za muhogo.

(b) Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004 wastani wa bei za muhogo ilikuwa Dola za Kimarekani 90 kwa tani ya muhogo uliokaushwa, Dola 158 kwa tani ya unga wa muhogo na Dola 82 kwa tani ya wanga wa muhogo.

(c) Mheshimiwa Spika, kiasi cha muhogo kinachosafirishwa kwenda katika masoko ya nje hutofautiana kutoka mwaka mmoja hadi mwaka mwingine kutegemeana na mahitaji ya wanunuzi. Kwa mfano, kati ya mwaka 1990 na 1995 Tanzania ilikuwa inasafirisha wastani wa tani 27,430 za muhogo kwenda kwenye soko la nchi za Ulaya. Mwaka 2003 tani 21.9 kwenda *DRC,* mwaka 2004 tani 302.7 kwenda Rwanda na mwaka 2005 tani 857.94 kwenda Rwanda, tani 11 kwenda Burundi na tani 4 kwenda *DRC.*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa mwaka 2004 nilileta mnunuzi wa muhogo tani laki 1 na Serikali ikanijibu kwamba nimshauri mnunuzi huyo ajenge kiwanda badala ya kununua muhogo, je, Serikali haioni kwamba maamuzi hayo yaliwarudisha nyuma wakulima wakati uzalishaji wa muhogo ni tani milioni 5 kwa Tanzania kutokana na takwimu alizotoa Naibu Waziri hivi sasa?

(b) Kwa nia hiyo ya Serikali ya kuwazuia wakulima hawa kupata soko la uhakika, je, Waziri haoni kwamba Serikali haikuwa na nia nzuri kwa wakulima wa muhogo hasa wa Mikoa ya Kusini ambao wangeweza kuongeza uzalishaji kutokana na uhakika wa soko?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE):** Mheshimiwa Spika, kuhusu ushauri wa Serikali wa kumwomba huyo mnunuzi kujenga kiwanda ulikuwa na nia njema tu kwamba itakapojenga kiwanda hapa cha kuweza kutengeneza mazao yanayotokana na muhogo itakuwa inaongeza thamani ya muhogo ili wakulima wetu waweze kunufaika zaidi na ndiyo maana katika majibu hapa nilipokuwa natoa bei za muhogo, ilionekana wazi kabisa kwamba bei ya zao la muhogo ghafi ni chini kuliko muhogo ule ambao ulikuwa umeishafanyiwa *processing*. Kwa hiyo, nia ya Serikali ilikuwa ni njema.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inakuwa na nia ya kuwazuia wakulima wasipate masoko, hiyo si kweli kwa sababu jitihada za Serikali ambazo nazifahamu kwa muda wote imekuwa ni kuwasaidia wakulima kuwatafutia masoko na mfano hai ni kwamba katika miaka hiyo ya 2001 hadi 2003 Serikali iliwahi kutuma ujumbe kutoka nchi za Mashariki ya mbali kwenda kutafuta masoko ya wakulima wa muhogo katika Mikoa ya Kusini, Mtwara na Lindi. *(Makofi)*

**MHE. ADAM K. A. MALIMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Katika majibu mazuri ya Naibu Waziri amesema kwamba zao la muhogo linalozalishwa Tanzania kwa kiasi kikubwa linakwenda nchi za jirani za Rwanda, Burundi na Congo. Lakini sehemu ya zao linalokwenda huko ni zao la muhogo linalolimwa katika Kanda ya Kigoma, Kanda ya Mkuranga, Rufiji mpaka chini huko Tandahimba na kadhalika, linazalisha sana zao la muhogo lakini halipati kupanua uzalishaji wake kwa sababu halina soko.

Je, Naibu Waziri anaweza kunisaidia ni kwa kiasi gani Serikali sasa itaangalia namna ya kuyaingia masoko haya ya Spain, Uholanzi na kadhalika ili na sisi wakulima wa Mkuranga pia na wengine wapate kuwa na uhakika kwamba zao lao litapata soko katika masoko hayo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE):** Mheshimiwa Spika, nimesema hapa wakati nikijibu swali la msingi kwamba mihogo yetu inauzwa katika masoko ya Jumuiya ya Ulaya na nikataja hiyo Spain ambayo Mheshimiwa Mbunge ameitaja. Kwa hiyo, jitihada za Serikali pamoja na kuainisha masoko ya muhogo yalipo ikiwepo na hiyo Spain, katika wakulima hawa wa Kusini, Mtwara, Lindi na Pwani nimeeleza hapa kwamba jitihada za Serikali ni kuwatafutia masoko na hivi sasa tunavyozungumza tayari kitengo cha masoko ambacho kipo katika Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kimeshaandaa utaratibu wa kufanya utafiti wa masoko ya mazao mbalimbali pamoja na mihogo na kutoa taarifa kwa wakulima wanaohusika ili waweze kujua masoko haya yako wapi.

Mheshimiwa Spika, lakini muhogo unaolimwa katika Mikoa ya Kusini licha ya kuuzwa nchi za nje, tunahimiza vile vile utumike kama chakula hapa nchini ili soko liweze kuwa la uhakika zaidi. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri aliyoyatoa Mheshimiwa Naibu Waziri, ningependa kutoa maelezo ya ziada kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika kuleta msukumo zaidi wa kilimo cha mazao hususan mazao ya chakula, Wizara yangu imekwishakamilisha mapendekezo ya kuunda chombo kwa jina la *National Grains and Food Crops Board* yaani Shirika ambalo ni la kiserikali litakalotoa uhakika wa masoko kwa mazao ya chakula ili tunapowahimiza wananchi kulima zao la muhogo au zao la mahindi au zao la mtama katika maeneo fulani, kuwe na uhakika wa soko na bei ambayo tutakuwa tunaitangaza mapema kabla ya mwanzo wa msimu kama *flow price* yaani bei ya kiwango cha chini ambacho Shirika hili litanunua bila kuzuia wanunuaji wa kibiashara kama watakuwa na bei za juu zaidi.

Mheshimiwa Spika, tunadhani tukiwa na chombo cha namna hiyo tutaweza kuhimiza kilimo cha muhogo kwa kujua soko lipo kama katika maeneo yale aliyoyazungumzia Mheshimiwa Mbunge ya Mkuranga, Mkoa wa Pwani na Mikoa ya Kusini. Chombo hicho kitanunua zao hili kwa bei ile iliyotangazwa na mkulima kila wakati atakuwa na uhakika kwamba soko la zao hilo lipo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira kwamba mapendekezo hayo yatafanyiwa uamuzi rasmi na sheria ya kuunda chombo hicho tunategemea itakuja hapa Bungeni na tutapata nafasi ya kutoa mawazo zaidi. *(Makofi)*

Na. 116

**Ahadi ya Serikali Kupeleka Maji kwenye Kata ya Itagano**

**MHE. BENSON M. MPESYA** aliuliza: -

Kwa kuwa Serikali iliahidi Bungeni kupeleka maji kwenye Kata ya Itagano, je, ni lini utekelezaji wa ahadi hiyo utaanza rasmi?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Benson Mpesya, Mbunge wa Jimbo la Mbeya Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kata ya Itagano ipo ndani ya mipaka ya Jiji la Mbeya ambalo linahudumiwa na Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Mjini Mbeya. Ina wakazi wapatao 1,232 kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2002. Mahitaji ya maji hivi sasa ni lita 74,000 kwa siku na yanatarajiwa kuongezeka hadi kufikia lita 96,000 kwa siku ifikapo mwaka 2015 ambapo idadi ya wakazi wakati huo inatarajiwa kufikia watu 2,600. Hivi sasa Kata ya Itagano haina huduma ya maji kutokana na eneo ilipo kutokuwa na chanzo cha maji wala mfumo wa kusambaza maji.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Majisafi na Majitaka katika Jiji la Mbeya imepata msaada wa kuboresha huduma ya majisafi na majitaka kutoka Serikali ya Ujerumaji kupitia Shirika lake la *KfW* na Jumuiya ya Ulaya *(EU)* unaogharimu shilingi

bilioni 7.1 kwa awamu ya kwanza na shilingi bilioni 29 kwa awamu ya pili. Utekelezaji wa awamu ya kwanza ulianza mwezi Mei, 2005 na unatarajiwa kukamilika mwezi Aprili , 2007. Kata ya Itagano imeingizwa katika awamu ya pili ya mradi huo. Awamu hiyo ina lengo la kuongeza upatikanaji wa maji katika Jiji la Mbeya kutokana na lita milioni 33 wakati awamu ya kwanza itakapokamilika hadi lita milioni 49.9.

Mheshimiwa Spika, tatizo la maji katika kata ya Itagano pamoja na kata za Mwamsekwa, Mwasanga na Tembela litakwisha baada ya kukamilika awamu ya pili ya mradi huu Desemba, 2009. Kwa kuwa katika awamu hiyo upanuzi wa chanzo cha maji cha Mfwiziko na ujenzi wa mfumo wa kusambaza maji katika kata nilizozitaja utakuwa umekamilika na utafanyika, hivyo kazi inayoendelea hivi sasa ni maandalizi kwa ajili ya uteuzi wa Mhandisi Mshauri atakayesanifu na kusimamia ujenzi wa mradi ambao umepangwa kuanza mwezi Machi, 2007.

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, nina swali dogo la nyongeza.

Kutokana na muda ambao umewekwa kwamba ni mpaka 2009 na ndugu zangu hawa hawajawahi kuwa na maji ya bomba toka tumepata Uhuru na kwa kuwa utafiti umefanyika kwamba chanzo cha maji kinaweza kutosheleza, ni kwa nini basi Serikali isiamue kutumia chanzo hicho ili iwe ni kama jibu la kuwapatia maji kwa muda mrefu kuliko kusubiri hadi mpaka huo mwaka 2009?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kutokana na jibu la awali kwamba tayari Itagano imo katika mpango wa kupatiwa maji itakapofika mwaka 2009, lakini pia nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba chanzo hicho ambacho tayari kipo kinaweza kikatumika. Lakini ningependa kumshauri Mheshimiwa Mbunge kwamba akashauriane na Halmashauri yake ya Manispaa ya Mbeya ili mpango huo wauingize katika miradi ya mpango wa majisafi, majitaka na mazingira katika awamu itakayofuata. *(Makofi)*

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa Spika, ahsante na ninashukuru pia kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri, lakini nina swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa tatizo la maji ni kero kwa maeneo mengi hapa nchini na baadhi ya maeneo wamefanya juhudi ya kujikomboa na tatizo hili hususan katika Kijiji cha Mpara, Wilaya ya Kilwa wametafuta wafadhili ambao wanaweza kuwasaidia kutatua tatizo hili ili wajikomboe. Je, Serikali itakuwa tayari kuwasaidia wananchi hao ili kuondoa tatizo hili katika eneo hilo? Ahsante.

**SPIKA:** Swali linaonekana kama la sehemu nyingine, lakini kama una majibu…

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki cha maswali nilijibu swali la Mbunge wa Kilwa Kusini, Mheshimiwa Hasnain Dewji, kuhusu mambo ya Mpara na pia tulisema kwamba Mpara imo katika kufadhiliwa na kushughulikiwa katika mambo ya maji. *(Makofi)*

Na. 117

**Kero ya Maji *Mabibo Hostel***

**MHE. HALIMA J. MDEE** aliuliza:-

Kwa kuwa kumekuwa na tatizo la maji kwa muda mrefu katika mabweni ya wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Mabibo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua tatizo hilo katika mabweni hayo pamoja na maeneo jirani?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Halima Mdee, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, mabweni ya wanafunzia wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam yaliyoko Mabibo hupata maji ya bomba kutoka kwenye mfumo wa maji unaotegemea mitambo ya kusukuma maji ya Ruvu Juu. Mitambo hiyo husukuma maji kutoka Mto Ruvu hadi kwenye matanki ya kuhifadhi maji yaliyoko Kimara. Kutoka Kimara maji hutiririka kwenye mabomba hadi maeneo ya Ubungo, Tabata, Mabibo na Ukonga.

Mheshimiwa Spika, mfumo wa maji kutoka Ruvu juu, kwa muda mrefu umekuwa ukikabiliwa na matatizo ya uchakavu wa mitambo, uhaba wa maji kwenye mto, pamoja na mfumo wa bomba usiotosheleza mahitaji. Hali hii imekuwa ikisababisha huduma ya maji kutolewa kwa mgao kwenye maeneo niliyoyataja, ikiwa ni pamoja na mabweni hayo ya Chuo Kikuu.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa maji katika hosteli hiyo, Shirika la Utoaji Huduma ya Maji Jijini Dar es Salaam *(DAWASCO)* limerekebisha ratiba yake ya mgao wa maji ili yaweze kufika kwenye mabweni hayo na maeneo ya jirani. Katika siku za hivi karibuni, mabweni ya Mabibo yameweza kupata maji kama ifuatavyo:-

* Ijumaa tarehe 10/3/2006 walipatiwa lita 162,000;
* Ijumaa tarehe 17/3/2006 walipatiwa lita 197,000; na
* Jumamosi tarehe 18/3/2006 walipatiwa lita 222,000.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo hawakuweza kutoa maji mpaka sasa kwa sababu mtambo wetu uliathirika kwa kuwa *transformer* inayoendesha mitambo ya Ruvu Chini kupigwa na radi tarehe 19/03 na kazi ya matengenezo ya *transformer* hiyo inaendelea na inatarajiwa kukamilika ifikapo tarehe 15 mwezi huu wa nne.

Mheshimiwa Spika, ikishakamilika ni kwamba maji kwenye *Hostel* hiyo tutaendelea na ratiba kama jinsi ambavyo tulikubaliana nao na ratiba hiyo tulikaa na

Mkuu wa *Hostel* na mimi nilikuwa ni mmojawapo ambaye tulijadili na kukubaliana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua hiyo ya upeo wa muda mfupi, Serikali kupitia *DAWASA* inatekeleza mradi wa ukarabati na upanuzi wa miundombinu ya maji Jijini Dar es Salaam. Mradi huo unadhaminiwa na Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Benki ya Uwekezaji ya Ulaya, *DAWASA* na *DAWASCO* kwa gharama ya Shilingi bilioni 164. Chini ya mradi huo ambao umepangwa kukamilika mwaka ujao 2007, kazi zifuatazo zitafanyika ili kuboresha huduma ya maji kwenye maeneo niliyoyataja:-

(i) Kununua na kufunga mitambo mipya ya kusukuma maji kwenye chanzo cha Ruvu Juu. Mitambo miwili imeagizwa nchini Austria kwa gharama ya Dola za Kimarekani 222,343 na inatarajiwa kuwasili nchini mwezi huu. Mitambo mingine minne imeagizwa nchini Pakistan kwa gharama ya Dola za Kimarekani 388,422 na inatarajiwa kuwasili nchini mwezi Agosti mwaka huu 2006.

(ii) Kubadili bomba kuu la kupeleka maji kwenye mtambo wa kusafisha maji wa Mlandizi. Kazi hii inaendelea na hadi sasa imefikia asilimia 35.

(iii) Kudhibiti uvujaji wa maji kwenye bomba kuu linalosafirisha maji kutoka Mlandizi hadi kwenye mantanki makubwa ya kuhifadhi maji yaliyoko Kimara. Hii ni pamoja na kufunga vifaa vya kuondoa hewa kwenye bomba mpya, kubadili viungio na kufunga dira za maji kwenye njia zote kubwa.

Aidha, chini ya mradi huu, maandalizi ya mpango wa muda mrefu wa kupanua mfumo wa maji ikiwa ni pamoja na uendelezaji wa vyanzo vipya vya maji unaandaliwa. Vyanzo vinavyochunguzwa ni mradi wa kutoa maji kutoka Mto Rufiji, Visima Virefu katika maeneo ya Mto Mpiji, Kizinga na Kigamboni na usanifu wa bwawa linalotarajiwa kujengwa kwenye Mto Ruvu eneo la Kidunda Mkoani Morogoro. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu yamebaki maswali mawili tu, nadhani ni busara kwamba niongeze muda kidogo ili tuyamalize haya. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu marefu ambayo mengine nilikuwa siyahitaji, nina maswali madogo mawili kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa amekiri kwamba *Mabibo Hostel* maji yanayopelekwa ni kwa Malori na ni tatizo la muda sana; ni lini *Mabibo Hostel* itapata maji ya moja kwa moja na sio kwa kutumia Malori?

(b) Tunafahamu *Mkapa Special Economic Zone* ipo jirani na *Mabibo Hostel* na kwamba pale maji yatakuwa yanapelekwa: Je, ni kwa kiasi gani Wizara yako imejiandaa kuhakikisha kwamba maji yatakayokwenda pale yatawanufaisha sio *Mabibo Hostel* tu bali na maeneo ya jirani? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, maelezo marefu yaliyotolewa ni kwa Bunge kuelewa kwa uhakika hatua zinazochukuliwa na Serikali katika kujibu tatizo la maji Dar es Salaam. Jiji la Dar es Salaam lina watu milioni tatu na nusu, lakini lina matatizo makubwa sana ya maji na Serikali inatambua hivyo. Kwa hiyo, hatua tunazozichukua zinagawanyika sehemu tatu. *(Makofi)*

Moja, ni hatua za muda mfupi za kukarabati miundombinu ya Dar es Salaam ili kuhakikisha maji yanayofika sasa kutoka Ruvu yanafika kwa sehemu kubwa zaidi kuliko ilivyo sasa kwa sababu ya kuondoa uvujaji unaofanyika njiani. Kwa hiyo, kama huondoi hilo huwezi kufikisha maji ya uhakika katika maeneo mengi ya Dar es Salaam. Hatua ya pili, ya muda wa kati ni kutengeneza visima ambavyo vitaunganishwa katika mfumo wa maji ya Dar es Salaam ambavyo vimetajwa na Naibu Waziri.

Hatua za muda mrefu ni za kutoa maji mto Rufiji ili kuhakikisha kwamba Dar es Salaam inapata maji ya uhakika katika kipindi cha muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunatambua kwamba kuna *economic zone* iliyo karibu na *Mabibo Hostel* na tumesema katika jibu letu kwamba pampu mpya ambazo zinafika tarehe 19 mwezi huu zitafungwa Ruvu na maji yataanza ku-*flow* na kiwango cha maji kitakachoanza kufika katika eneo hilo kitaongezeka pamoja na maeneo mengine ya Ubungo, Tabata na *Airport.* Kwa hiyo, majibu marefu yalikuwa lazima kwa maswali muhimu. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI**: Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji kwa majibu mazuri aliyoyatoa hapa Bungeni. Lakini vile vile namshukuru Mheshimiwa Waziri wa Maji kwa kujibu vizuri maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Mdee. Naomba kwa niaba ya Waziri wa Maji, niongezee ile hoja aliyoisema Mheshimiwa Mbunge kuhusu *size* ya tanki la maji la Mheshimiwa Benjamin William Mkapa ambayo tunaijenga katika eneo la Mabibo.

Tanki la Maji la *size* ile litafikia uwezo wa kuchukua maji lita milioni nne. Kwa hiyo, tumeshakubaliana na *Mabibo Hostel* kwamba maji yao pia watapata kupitia tanki lile ambalo liko katika eneo hilo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Nkayamba umeniandikia kulalamika, lakini ilihusu Mabibo au maeneo ya karibu?

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali. Lakini swali langu linafanana na *Mabibo Hostel* hiyo hiyo. Kwa kuwa swali langu linafanana na la Mheshimiwa Mbunge aliyetangulia na kwa kuwa wanafunzi wa Mkoa Kigoma ambao wanakaa Hosteli wamekuwa na shida ya maji kwani wamekuwa wakiamka alfajiri kwenda kutafuta maji katika Ziwa Tanganyika: Je, Serikali ina mpango gani kuhusu wanafunzi hao ambao wanaamka alfajiri kwenda kutafuta maji hasa wasichana wakati Ziwa Tanganyika huwa halikauki? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, una hiari ya kujibu tumehamia Ziwa Tanganyika, lakini ni matatizo ya wanafunzi. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Mbunge atuletee swali jipya ili tuweze kumjibu kwa uhakika. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. AMINA CHIFUPA MPAKANJIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimpongeze Waziri kwa majibu mazuri aliyoyatoa. Hata hivyo nina swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa tatizo la maji kwa Mkoa wa Dar es Salaam ni la muda mrefu pamoja na maeneo ya Chuo Kikuu na maeneo jirani, lakini kwa mshangao wakazi hawa wa Dar es Salaam wamekuwa wakiletewa *bills* kila mwisho wa mwezi na *DAWASCO*: Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kuwashauri *DAWASCO* waache kufanya usumbufu huu ambao wanawaletea wateja kwa kuwaletea bili wakati hawapati maji? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba wakazi wote wa Dar es Salaam, nikiwemo hata na mimi hata na Waziri wangu pia tunapata bili za maji. Bili za maji siyo kwamba ni kwa ajili ya yale unayokunywa peke yake, pia kuna gharama nyingi ambazo ndio zinajumuishwa mtu unapata bili ya maji. Lakini hata hivyo kwa hivi sasa kero hiyo tunaiondoa kwani *DAWASA* na *DAWASCO* wameshaanzisha *Billing System* mpya na imefungwa na ambayo sasa itakuwa na uhakika kwamba mteja atalipa maji kufuatana na kile alichotumia. Ahsante. *(Makofi)*

Na. 118

**Ushuru wa Forodha kwa Nchi za Afrika Mashariki**

**MHE. JOB Y. NDUGAI** aliliuza:-

Kwa kuwa ushuru wa Forodha kwa nchi za Afrika Mashariki umeanza kutumika tarehe 01 Januari, 2005:-

(a) Je, Tanzania inafaidikaje?

(b) Je, kumekuwapo ukiukwaji wowote unaofanywa na Kenya na Uganda?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO KIMATAIFA (k.n.y WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ningependa kujibu swali la Mheshimiwa Job Ndugai, Mbunge wa Kongwa, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Faida za ushiriki wa Tanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki zinatokana na Itifaki ya Umoja wa Forodha na malengo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa hiyo, Tanzania inafaidika:-

Mosi, kwa kuuza bidhaa zake Kenya na Uganda bila kulipiwa ushuru kabisa jambo ambalo halikuwepo hapo awali;

Pili, kuongezeka kwa ajira kwa wananchi kutokana na kuongezeka kwa uzalishaji uliosababishwa na kupanuka kwa soko na bidhaa kutolipwa ushuru;

Tatu, kuvutia wawezekaji wakubwa katika soko la Afrika Mashariki; na

Nne, kuongezeka kwa ufanisi kutokana na nchi wanachama kuzalisha katika maeneo yale ambayo wana uwezo nayo *(Comparative advantage).*

(b) Mwanzoni mwa utekelezaji wa Itifaki ya Umoja wa Forodha yalijitokeza matatizo ya kiutekelezaji na si ukiukwaji wa Itifaki hiyo kwa makusudi. Mathalan, viwango vya kodi katika mitumba vilipanda sana kiasi cha kukosa uwiano kati ya mahitaji na upatikanaji kiasi cha kusababisha malalamiko mengi kutoka kwa wananchi wa nchi zote tatu. Kwa hiyo, marekebisho ya ushuru yalihusu nchi zote kwa upande wa mitumba. Aidha, Jumuiya imejiwekea taratibu zinazoruhusu nchi wanachama kuwasilisha mapendekezo ya kubadili viwango vya ushuru wa forodha kwa baadhi ya bidhaa zinazotoka nje ya nchi mwanachama wa Jumuiya au kuahirisha utekelezaji wake. Kwa mfano, Uganda iliomba na kuruhusiwa kutokutekeleza wigo wa pamoja wa ushuru kwa malighafi za viwandani kwa kipindi cha miaka mitano. Vile vile, Kenya ilikubaliwa kusitisha matumizi ya wigo wa pamoja wa ushuru katika mchele kwa kipindi cha miezi 24 na vivyo hivyo Tanzania kwa upande wa mahindi na mchele ili kukabiliana na upungufu wa chakula kutokana na ukame ulioikumba nchi yetu kuanzia mwishoni mwa mwaka jana, 2005.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Kenya na Uganda walikaidi kufuata viwango walivyokubaliana katika Afrika Mashariki vya ushuru wa madawa *(Common External Tariffs)* na kwa namna hiyo wametutia hasara Tanzania:-

(a) Je, Serikali inasema nini kusema jambo hilo?

(b) Kwa vile jambo hili la ushuru wa forodha ni jambo ambalo ni muhimu sana kwa ushirikiano wetu wa Afrika Mashariki: Je, Serikali inachukua hatua gani za kuwaelimisha Watanzania ili hata wananchi wa kule Kongwa, Nali, Kibaigwa na maeneo mengine waweze kutumia fursa ambazo zimo katika jambo hili ambalo bado halieleweki vizuri kwa Watanzania wengi? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI (k.n.y WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI):** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa majibu mazuri ambayo ameyatoa hapa Bungeni. *(Makofi)*

Kuhusu swali la Mheshimiwa Job Ndugai kuhusu nchi ya Kenya kukiuka makubaliano kuhusu madawa, suala hili tumeshalizungumza kwenye Baraza la Mawaziri wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na muafaka umepatikana. Ni kweli kama alivyosema

Mheshimiwa Naibu Waziri, kwamba kila nchi pamoja na kwamba tuna ule Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wa biashara *(the Customers Union Protocol)* lakini kuna mambo ambayo nchi inashindwa kutekeleza kwa sababu ya hali halisi ya uchumi wa nchi. Kwa hiyo, wanaweza wakachukua hatua ambayo inaahirisha utekelezaji wa maamuzi yale. Lakini mradi mnafuata utaratibu na utaratibu ni kwamba lazima mrudi kwenye Baraza na mnazungumza na mkubaliana, kwa hiyo, kutokana na hilo siyo tena tatizo kubwa kama lilivyokuwa pale awali.

Kuhusu swali la pili la kuelimisha wananchi, hili tunasema siku zote hata hapa Bungeni tumefanya Semina kuelezana umuhimu wa kuwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa sababu gani? Kwanza linapanua soko. Soko letu kubwa zaidi linawezesha wawekezaji kutoka nje na ndani ya nchi kuwekeza katika viwanda au katika kilimo kwa kutarajia soko lililokuwa kubwa la Afrika Mashariki ambalo lina watu zaidi ya milioni mia moja. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tuendelee kuwaeleza wananchi faida tuyopata kutokana na Jumuiya ya Afrika ya Mashariki.

Lakini tatu, vile vile kuuza bidhaa zetu kwa mfano Kenya inaanza kupata matatizo ya ukame na ilitokea mwaka jana, 2005 kwamba sisi Watanzania huku tuliuza mahindi mengi kwa bei nzuri zaidi Kenya. Kwa hiyo, kuwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki inatusaidia kupanua soko kwa maana ya biashara, lakini vile vile soko kwa maana ya uwekezaji. *(Makofi)*

Na. 119

**Uagizaji wa Chakula cha Mifugo**

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA** aliuliza:-

Kwa kuwa kutokana na ukame unaoendelea sana katika baadhi ya maeneo ya nchi yetu, Serikali imeanza kuagiza chakula toka nje ya nchi na kukisambaza kwa wananchi wahitaji na kwamba kusambazwa kwa chakula hicho kunaweza kuendelea pengine hadi mvua za msimu ujao na kwa kuwa hali hiyo ya ukame imeathiri pia mifugo:-

(a) Je, Serikali ina mipango yoyote ya kuagiza vyakula kwa ajili ya mifugo yetu toka nje ya nchi kama inavyoagiza dawa za mifugo na kukisambaza kwa wafugaji ili wakinunue na kuilisha mifugo yao kwa lengo la kuinusuru mifugo hiyo?

(b) Kwa kuwa ukame huo umesababisha pia upungufu wa maji ya kunyweshea mifugo hiyo: Je, Serikali itachukua hatua gani kukabiliana na tatizo hilo na kuwasaidia wafugaji?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mhonga, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli ukame wa mwaka 2005/2006 umeathiri kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa malisho na maji ya mifugo nchini. Hali hiyo imesababisha ng'ombe 115,121, mbuzi 133,237, kondoo 122,069 na punda 744 kufa. Aidha, kutokana na kudhoofika kwa mifugo, baadhi ya wafugaji walilazimika kuuza mifugo kwa bei za chini sana kama vile Sh.15,000/= kwa ng'ombe na Sh.2,000/= kwa mbuzi na kondoo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na wingi wa mifugo iliyopo nchini na gharama kubwa ya vyakula vya mifugo na ufinyu wa Bajeti ya Wizara yangu, Serikali haitaweza kuagiza vyakula vya mifugo toka nje ya nchi. Hata hivyo, kwa neema za Mwenyezi Mungu mvua zimenyesha vizuri karibu nchi nzima na kwa hiyo, hatuna haja tena hivi sasa kuagiza vyakula vya mifugo. Lakini kwa matumizi ya siku za baadaye, Serikali ina mpango wa kuwashawishi na kuwahimiza wafugaji, Halmashauri za Wilaya, Taasisi na watu binafsi kuanzisha mashamba ya kibiashara ya malisho ya mifugo ambayo yanaweza kuzalisha nyasi za kutosha zitakazoweza kuvunwa na kuhifadhiwa kwa ajili ya matumizi wakati wa kiangazi ama ukame wowote. Vile vile Serikali inahamasisha uwekezaji katika viwanda vya vyakula vya kutosheleza mahitaji yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kwamba kuna upatikanaji mzuri wa mbegu za malisho, Serikali itaimarisha mashamba ya mbegu za malisho ya Langwira Mbeya na Vikuge Pwani yaliyopo chini ya Wizara yangu na kuanzisha mengine kutegemeana na mahitaji. Tunaiomba pia sekta binafsi iunge mkono juhudi hizo za Serikali. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na uhaba wa maji wakati wa kiangazi na ukame, Wizara yangu imejiwekea utaratibu wa kuchangia gharama za ujenzi na ukarabati wa malambo nchini kwa uwiano wa asilimia 50 inayotolewa na Wizara, Halmashauri asilimia 30 na kwa wananchi kuchangia asilimia 20.

Kupitia utaratibu huu tangu mwaka 2001/2002 mpaka sasa, Wizara imechangia jumla ya Shilingi bilioni 1.054 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa malambo 326. Kutokana na ukame uliojitokeza, Wizara yangu imepanga kupanua mpango huo kuanzia mwaka huu, 2006 kwa kuchimba malambo makubwa zaidi ambayo yataombewa fedha Serikalini katika Bajeti yake ya mwaka 2006/2007. Jitihada hizi zinatarajiwa pia kuondoa tatizo la wafugaji kuhamahama kutoka sehemu moja ya nchi kwenda nyingine wakitafuta maji kama ilivyotokea siku za hivi karibuni. *(Makofi)*

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuuliza maswali mawili kama ifuatavyo:-

(a) Katika swali la msingi Mheshimiwa Naibu Waziri, amejibu kwamba watahamasisha Halmashauri na watu binafsi kuanzisha mashamba kwa ajili ya malisho. Je, isingekuwa vyema kwa Serikali kutoa ruzuku kwa wafugaji hao ili waweze kulima wenyewe mashamba kwa ajili ya majani ya malisho ya mifugo yao?

(b) Nchi nyingine kwa mfano Malaysia wameweza kutengeneza mvua kwa *chemicals.* Je, Serikali ya Tanzania ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba hatutapata

tatizo tena la ukame ikiwa tatizo la ukame limekuwa likijitokeza mara kwa mara na mvua ya *chemical* inaweza ikasaidia kuondoa tatizo hilo kabisa? *(Kicheko)*

**SPIKA:** Hili la pili naona ni swali jipya la namna ya kutengeneza mvua. Lakini la kwanza Mheshimiwa Naibu Waziri jibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, tunaamini wafugaji wanaweza wakaanzisha mashamba yao ya malisho kwa sababu inahitaji tu upatikanaji wa mbegu . Kwa taarifa, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa siku za karibuni nilitembelea shamba la mbegu za malisho la Vipuge, wananchi wengi waliniona kwenye luninga na wakaanza kunipigia simu kwamba tunazihitaji hizo mbegu. Kwa hiyo, wananchi wako tayari hawajaomba kusaidiwa isipokuwa wanazihitaji hizi mbegu na zinapatikana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wakati Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu akijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa John Malecela, Mbunge wa Mtera, lililohusiana na swali la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Swali Namba 105 ilidhihirika kwamba yalitakiwa maelezo ya kina zaidi kuliko yale yaliyotolewa. *(Makofi)*

Napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na Serikali. Huu ni utaratibu mzuri na mimi kama Spika nitazingatia majibu ya ziada yanapopatikana ni vizuri yatolewe kwa sababu nia ya Bunge na wananchi ni kujua kwa undani nini kinachoendelea. Kwa maana hiyo, naomba sasa Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu, ambaye ameniletea taarifa hapa baada ya kuwa amechakarika katika kipindi hiki cha maswali mpaka akauliza Dar es Salaam, sasa ana majibu na sasa majibu yatolewe. Mwanasheria Mkuu karibu. *(Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii kutoa majibu ya ziada kuhusiana na lile swali lililoulizwa na Mheshimiwa John Samwel Malecela.

Mheshimiwa Spika, nimeshapata taarifa kamili kuhusiana na zile kesi mbili ambazo Mheshimiwa Malecela aliziulizia. Kwa kasi mpya nilitoa maagizo kwenye Ofisi yangu ya Dar es Salaam waniletee taarifa hii. Ninashukuru kwamba kwa muda mfupi chini ya saa moja taarifa ilifika hapa Dodoma kutoka Dar es Salaam. Shauri aliloulizia Mheshimiwa John Malecela lilihusu kesi ile ya *Mbezi Beach*. Kesi ile ya *Mbezi Beach* iliwahusu watu wafuatao, nao ni:- Jonathan Lolangwai Elihu, Hamad Salum Mtingo, Benedict Marks, Pantaleo Miyeya Mjwahuki, Damson Aniel Munisi na Jonas Bulai.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hukumu ya kesi hii ilitolewa tarehe 30 mwezi Desemba, 2005 washtakiwa wawili Daniel Aniel Munisi na Jonas Bulai walionekana wana hatia kwa makosa waliyoshitakiwa nayo. Daniel Aniel Munisi alionekana ana hatia na kuhukumiwa kifungo cha miaka kumi jela na Jonas Bulai alionekana ana hatia akahukumiwa kifungo cha kulipa faini ya Shilingi milioni tano.

Mheshimiwa Spika, Mkurugenzi wa Mashitaka hakuridhika na adhabu zilizotolewa dhidi ya Jonas Bulai na ameomba rufaa Mahakama ya Rufaa ya Tanzania. Pia, hawa washitakiwa wengine wa kwanza, wa pili, wa tatu mpaka wa nne walionekana hawana hatia lakini Mkurugenzi wa Mashitaka anafikiri kwamba hakuridhika na hukumu hiyo. Kwa hiyo, ameomba rufaa Mahakama ya Rufaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu kesi ya Akasha, hiyo kesi ilikuwa ni ya siku nyingi sana, kwa bahati mbaya mpaka sasa hivi bado wanaendelea kutafuta kumbukumbu za hiyo kesi ya Akasha. Kwa hiyo, tutakapopata kumbukumbu zake tutampatia Mheshimiwa John Malecela na tutakapopata kumbukumbu zote za kesi ya Akasha tutaliarifu Bunge lako lijalo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana na mimi nitahakikisha nitakupa nafasi mapema kabisa katika Mkutano ujao wa Bunge ili waweze kupata majibu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kuna matangazo machache tu. Kwanza tumepata taarifa kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu ya kustakabadhi, kupokea fedha zilizochangwa na sisi sote Wabunge ili ziingie katika Mfuko wa Kukabiliana na Njaa, ule Mfuko wa Taifa. *(Makofi)*

Taarifa hii Ofisi ya Waziri Mkuu imepokea hundi yetu ya jumla ya Sh.12,760,000/= ukiwa ndiyo mchango wa Wabunge katika hili baa la njaa lililotufika katika Taifa. Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kujitoa kwenu na kuonyesha kwa wananchi kwamba tuko pamoja nao. *(Makofi)*

Tangazo la pili, Mkutano wa Kwanza wa Tume ya Huduma za Bunge, Mkutano muhimu sana, utafanyika Ofisini kwangu leo saa 6.30. Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati msifanye haraka ya kwenda Dar es Salaam, ni Kikao kifupi lakini ni muhimu sana, kwa sababu kinazungumzia huduma za Bunge hili. Saa 6.30 *Board Room* ya Spika.

Waheshimiwa Wabunge tangazo la tatu, jana tulipokuwa tunawaenzi wale vijana waliofanya vizuri katika riadha na kuiletea nchi yetu heshima kulitokea baadhi ya Wabunge kwa sababu Spika ana masikio mapana, waliolalamika kwamba sikumwita Mtoa Hoja ili tena tuhoji ili tukubali hoja ya kuwapongeza wale vijana. Nilikuwa napenda kufafanua kwamba hapa sio kwamba kulikuwa na kosa lolote. Umejengeka utamaduni ndani ya Bunge hili kwamba kwa hoja za namna hii za kupongezana na ambazo wala hazipo katika maandishi, hoja ya Bunge inabidi iwe ni *addendum* kwenye *Order Paper* ndiyo hoja rasmi hiyo.

Sasa nimeendelea kuukubali utamaduni kwamba inapotokea kwamba tunampongeza tu Mtanzania yeyote kwa mema aliyofanya inatosheleza yale tuliyoyafanya. Sio lazima liletwe na Mtoa Hoja ombi la hoja ambalo Mheshimiwa Spika awahoji tena Wabunge. Nadhani utaratibu huu unatosheleza na napenda kuthibitisha kwamba umo ndani ya Kanuni na isitoshe *Hansard* inachukua yote. Kwa hiyo, kumbukumbu hizo zinabaki daima kwa Watanzania. Ahsante sana. *(Makofi)*

**ND. JAPHET M. SAGASII - KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa Taarifa kwamba shughuli zote zilizokuwa zimepangwa kwa ajili ya Mkutano huu wa tatu, sasa zimemalizika.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kutokana na taarifa hiyo ya Katibu kwamba shughuli zote zilizopangwa kwa Mkutano huu sasa zimemalizika, ninayo heshima sasa kumwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu atoe hoja ya kuahirisha Bunge. *(Makofi)*

**KUAHIRISHA BUNGE**

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kutekeleza majukumu yetu katika muda wote tuliokuwa hapa Dodoma.

Katika Mkutano huu maswali 119 ya Waheshimiwa Wabunge yamejibiwa na Serikali. Majibu ya maswali hayo yameiwezesha Serikali kutoa ufafanuzi wa maeneo muhimu ambayo Waheshimiwa Wabunge walipenda kujua maendeleo na utekelezaji wake. Naamini, kwa kupitia majibu hayo, wananchi wameweza kujua mipango, mikakati na maamuzi mbalimbali ambayo Serikali imechukua katika kutekeleza majukumu yake, hasa yale yanayohusu na kugusa maendeleo yao.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu, Bunge lako Tukufu limepitisha miswada miwili. Miswada hiyo ni ule uliopendekeza kutungwa kwa Sheria ya Benki Kuu ili kukidhi matakwa ya wakati huu ya utekelezaji wa majukumu ya Benki Kuu yanayohusu Sera za fedha. Muswada wa pili ni ule uliopendekeza kuifuta Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha na kutunga Sheria mpya ya mwaka 2006. Miswada yote miwili ilijadiliwa kwa umakini na Waheshimiwa Wabunge na kutoa mawazo yao yaliyowezesha kuboreshwa kwa miswada hiyo.

Mheshimiwa Spika, napenda niwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kukubali kupitisha miswada hiyo. Hii ni hatua muhimu sana kwa Serikali ya kutekeleza kwa dhati mageuzi makubwa katika Sekta ya Mabenki na Taasisi za Fedha nchini. Natumia fursa hii kukushukuru sana wewe mwenyewe kutoa nafasi ya kutosha kwa Waheshimiwa Wabunge kuchangia miswada hii. Changamoto na ushauri uliotolewa tumeupokea.

Ninawahakikishia kuwa Sekta ya Fedha itaendelea kuimarishwa ili iweze kukabili ipasavyo changamoto ya huduma na kupanuka kwa uchumi wa Taifa letu. Miongoni mwa mambo yatakayopewa kipaumbele na Benki Kuu ni suala la riba za Mabenki kwa mtazamo wa kupunguza tofauti kubwa baina ya riba kwa mikopo na riba kwa amana. Lengo ni kuwezesha wananchi wengi Vijijini na wale wa kipato cha chini waweze kunufaika zaidi na mikopo midogo inayotolewa na Mabenki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki cha Bunge, tulifanya uchaguzi wa Wawakilishi katika Taasisi tatu muhimu za humu nchini. Napenda nitumie nafasi hii

kumpongeza Mheshimiwa Dr. Binilith Satano Mahenge - Mbunge wa Makete, kwa kuchaguliwa kuwa Mwakilishi wa Bunge katika Bodi ya Taasisi ya Sayansi na Teknolojia - Mbeya. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Aggrey Deaisile Joshua Mwanri, Mbunge wa Siha, kwa kuchaguliwa kuwa Mwakilishi katika Bodi ya Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere na pia nampongeza Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mbunge wa Muyuni, kwa kuchaguliwa kuwa Mwakilishi katika Bodi ya Vyuo Vikuu vya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yangu ya kufunga Mkutano wa Pili wa Bunge lako Tukufu, nilielezea juu ya tatizo kubwa la ukame ambalo lilisababisha upungufu mkubwa wa chakula nchini. Aidha, tulishuhudia ukosefu wa mvua kwa kipindi kirefu ambao ulituathiri sana kiuchumi. Mheshimiwa Rais katika hotuba yake alipozungumza na wananchi kutokea hapa Dodoma tarehe 31 Machi, 2006 alieleza mengi ambayo Serikali tayari imefanya katika kukabiliana na tatizo hilo.

Napenda nimshukuru Rais, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kutuongoza vizuri kukabili matatizo yaliyotukumba katika kipindi hiki na hivyo kuiwezesha Serikali kukakabiliana na hali kama hiyo. Nawashukuru pia kwa dhati wale viongozi na waumini wa dini mbalimbali walioombea nchi yetu ipate mvua za kiasi. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kusikiliza maombi yetu. Tumejifunza nini? Tumejifunza mengi, hasa masuala ya utendaji wetu katika kutatua matatizo ya wananchi. Tumetambua vilevile umuhimu wa kushirikiana katika kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa mambo muhimu ya kitaifa wakati wa matatizo. Tumejifunza kuwa wananchi wetu ni wavumilivu! Wanajua kusadiana na kuhifadhiana wakati wa dhiki. Tumeona ufanisi wa kiutendaji wa viongozi wetu pamoja na matatizo yanayowakabili. Wengi wa viongozi wetu wamefanya vizuri katika kipindi hiki. Tunawapongeza na kuwashukuru wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia, tatizo hili la ukame limetuwezesha kubaini udhaifu katika uongozi na utendaji. Kwa mfano, tumeshuhudia baadhi ya Watendaji wakikiuka taratibu tulizojiwekea katika ugawaji wa chakula cha msaada. Napenda nitoe mifano michache. Mkoani Arusha wapo Maafisa Watendaji ambao waliamua kuuza mahindi ya msaada kwa bei walizojipangia. Hawa wamesimamishwa kazi na wamefunguliwa mashtaka. Huko Arusha vile vile yupo aliyeamua kuficha magunia 25 ya mahindi, huyu amefunguliwa mashtaka na kusimamishwa kazi. Katika Mkoa wa Kagera, Wilaya ya Biharamulo, Mwanakamati wa Kamati ya Ugawaji aliiba mahindi ya msaada kilogramu 72. Wanakijiji walimkamata pamoja na mahindi hayo, wakamfungulia mashtaka na kuhukumiwa kifungo cha miaka mitano Gerezani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wa Lindi, Maafisa watano walihusika na upotevu wa magunia 96 ya mahindi kutoka katika ghala la Taifa la kuhifadhi chakula. Wametakiwa wafidie mahindi hayo na wamefanya hivyo. Hivi sasa wamefunguliwa mashtaka ya uzembe. Kule Tabora, Mtendaji wa Kijiji alitoroka na Sh. 550,000/= sawa na magunia zaidi ya 120 ya mahindi. Huyu amekamatwa na amefunguliwa mashtaka ya wizi na utoro kazini. Wajumbe wa Kamati ya Maafa ya Kijiji cha Sungwizi Wilaya ya Igunga wamefikishwa Mahakamani kwa mashtaka ya wizi wa mahindi yenye thamani ya

Sh.115,000/= sawa na magunia 25 ya mahindi. Katika Mkoa wa Dodoma Wilaya ya Mpwapwa Kata ya Mlunduzi, Mtendaji wa Kijiji pamoja na Mratibu wamehusishwa na wizi wa magunia mawili na nusu ya mahindi ya msaada. Mashauri yao yako Polisi na upelelezi unaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mifano hiyo michache katika baadhi ya Mikoa inaonesha upungufu wa uadilifu kwa baadhi ya Watendaji na Viongozi wanaopewa dhamana ya kuwasaidia wananchi. Tunapopewa Uongozi, hususan katika wakati wa matatizo kama tuliokuwanao, ni wajibu wetu kuweka mbele maslahi ya wale tunaowaongoza. Wito wangu kwa Viongozi na Watendaji ni kuwa tuwe Waadilifu katika utendaji kazi. Tuendelee kukemea na kuzichukulia hatua tabia chafu kama hizi. Naungana na kauli ya Mheshimiwa Rais kwamba tusiwaonee huruma watu hao wachache wanaofanya vitendo kama hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tarehe 23 Januari, 2006 nilipofungua Semina ya Wabunge pale Mjini Dar es Salaam, nilizungumzia juu ya hali ya matokeo mabaya ya Elimu ya Msingi. Nilitoa mifano ya Mikoa ambayo haikufanya vizuri katika kuwapatia nafasi wanafunzi waliofaulu Elimu ya Sekondari katika Mikoa ya Dar es Salaam, Mbeya, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Mtwara na Kigoma. Mikoa hiyo ndiyo iliyokuwa imeshindwa kuwapatia nafasi ya kuingia Sekondari angalau asilimia 50 ya wanafunzi waliofaulu mtihani wa Taifa wa Darasa la Saba. Baada ya Mkutano ule tulikaa na Viongozi (wakiwemo Wabunge) wa Mikoa kadhaa na kukubaliana kuibadili hali hiyo. Lazima nikiri walionigutua ni Wabunge wa Mkoa wa Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba tumepata mafanikio makubwa. Kwa mfano, Mkoa wa Dar es Salaam, katika uchaguzi wa mwanzo uliweza kuwapeleka Sekondari asilimia 21.7 tu ya wanafunzi waliofaulu lakini sasa umeongeza wanafunzi 10,660 na kufikia asilimia 70.2 ya waliofaulu. Mkoa wa Dodoma ulikuwa na asilimia 47.8 umeongeza wanafunzi 3,520 na kufikia asilimia 75.2 ya waliofaulu. Mkoa wa Mbeya ulikuwa na asilimia 30.1 umeongeza wanafunzi 7,240 na kufikia asilimia 56.1. Mkoa wa Mtwara ulikuwa na asilimia 44.2 umeongeza wanafunzi zaidi 1,760 na kufikia asilimia 63.1 ya waliofaulu. Mkoa wa Shinyanga ulikuwa na asilimia 34.2 umeongeza wanafunzi zaidi ya 7,693 na kufikia asilimia 69.9 ya waliofaulu. Mkoa wa Singida ulikuwa na asilimia 39.8 umeongeza wanafunzi zaidi ya 4,141 na kufikia asilimia 87. Mkoa wa Tabora ulikuwa na asilimia 33.7 umeongeza wanafunzi zaidi 3,814 na kufikia asilimia 77 ya waliofaulu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, takwimu hizi zinaonyesha juhudi ambazo zimefanywa na Viongozi wa Mikoa hii katika kipindi kifupi cha miezi mitatu kwa kuweza kujenga madarasa zaidi na Shule mpya za Sekondari. Hivi sasa kwa kutumia takwimu hizi za Mikoa minane tumeweza kuongeza wanafunzi zaidi ya 50,715 ambao wametuvusha kutoka asilimia 45 ya wanafunzi waliokuwa wamechaguliwa Awamu ya Kwanza mwezi Desemba, 2005 hadi kufikia asilimia 62.5. Hizi ni dalili nzuri katika Sekta ya Elimu. Lakini bado tusiridhike tulipofikia kwa kuwa wapo wanafunzi waliofaulu lakini hawajapata nafasi. Ilani ya Uchaguzi ya CCM inaelekeza kuwa ifikapo mwaka 2010 tuweze angalau kuwaingiza Sekondari asilimia 50 ya watoto wanaofaulu Elimu ya

Msingi. Kwa msukumo huu tuliouanza, nina hakika tutafikia malengo na kuyavuka. Wito wangu ni kuwa tusilegeze kamba na twende kwa kasi hii tuliyoanza nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza sana Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Mheshimiwa Margaret Sitta na timu yake ya Wizara kwa kazi kubwa waliyoifanya. Aidha, nawapongeza Wakuu wa Mikoa yote waliosukuma maendeleo katika Mikoa minane iliyohusika na zoezi hili. Nikianzia na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam - Mheshimiwa Yusufu Makamba, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma - Mheshimiwa William Lukuvi, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya - Mheshimiwa John Mwakipesile, Mkuu wa Mkoa wa Mtwara - Mheshimiwa Henry Daffa Shekiffu, Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga - Mheshimiwa Brigedia Jenerali Dr. Jones Balele, Mkuu wa Mkoa wa Singida - Mheshimiwa Parseko Ole Kone na Mkuu wa Mkoa wa Tabora Mheshimiwa Ukiwaona Ditopile Mzuzuri.

Nawapongeza wao na Viongozi wenzao waliosaidiana kuikamilisha kazi hii. Ni dhahiri kwamba, kumbe tukijipanga vizuri tunaweza kufanya mambo kwa muda mfupi na yenye matokeo yanayoonekana. Changamoto tuliyonayo ni kuendeleza ujenzi wa madarasa zaidi, nyumba za Walimu, Maabara na vyoo vya kutosha kwa ajili ya wanafunzi wetu. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ifanye utaratibu wa dharura kuhakikisha kwamba Shule zote mpya zinapatiwa Walimu haraka ili wanafunzi waliochaguliwa kuingia katika Shule hizo waanze mafunzo. Wakuu wa Mikoa kwa kushirikiana na Wizara wahakikishe nyumba za Walimu pia nazo zinakamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kusisitiza umuhimu wa kuwekeza katika elimu. Elimu ya kutosha ni jambo muhimu hata katika shughuli za kila siku za mtu yeyote. Elimu inamsaidia mtu kubuni, kupanga vizuri na kutekeleza kwa ufanisi shughuli za maendeleo yake na familia yake na hatimaye maendeleo ya jamii inayomzunguka. Elimu kama alivyosema Baba wa Taifa letu ni mkombozi.

Mtu aliyeelimika ana uwezo wa kufanya maamuzi sahihi ya wakati gani na wapi atafute ushauri wa kutekeleza malengo aliyojiwekea. Maisha ya baadaye yanategemea maandalizi ya sasa. Tuwahimize wananchi wetu watumie rasilimali zao kuwekeza katika elimu ya watoto wao. Bila elimu, itakuwa vigumu kupata kazi katika soko la ajira. Tusipowekeza katika elimu itakuwa vigumu kupata kazi katika soko la ajira. Tusipowekeza katika elimu ya watoto sasa, watoto wetu baadaye watakuwa wakata kuni na wateka maji katika soko pana la ajira la Afrika Mashariki; Afrika na duniani. Tuwahimize wananchi kuchangia katika maendeleo ya elimu ya watoto wao kama tunavyochangia katika harusi na maeneo mengine ya shughuli za marafiki na familia zetu. Tuwaelimishe Wananchi kupunguza matumizi katika sherehe na anasa na badala yake kutumia rasilimali zao katika kuwekeza katika elimu ya watoto wao. Waziri Mkuu wa Uingereza, Bwana Tony Blair aliwaambia wananchi wake nanukuu:

"Napenda wale Wazazi ambao hawana ndoto tena ya kwenda Chuo Kikuu, mategemeo yao yawe kwa watoto wao." Mwisho wa kunukuu. Hilo ndilo tegemeo kubwa la kizazi cha wakati huu. Wengi wa wazazi hawategemei kusoma tena Chuo Kikuu kwa sasa, lakini watoto wao wanaweza kama wakiandaliwa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukame mkubwa uliosababisha upungufu wa chakula umetupa changamoto kubwa kuhusu umuhimu wa kuleta mabadiliko makubwa katika mazingira na kilimo chetu. Napenda kuwaomba viongozi na wananchi tuzingatie maelekezo ya Serikali yaliyotangazwa na Makamu wa Rais Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein kuhusu uhifadhi wa mazingira nchini. *(Makofi)*

Kwa upande wa kilimo, hatuna budi sasa tuzalishe kwa wingi na kuweka akiba ya chakula kuanzia ngazi ya kaya hadi ngazi ya Taifa. Hivi sasa mvua zinanyesha katika maeneo mengi nchini. Habari kutoka Mikoa mingi nchini zinaonyesha kuwa kuna hali nzuri ya mvua na maji yapo ya kutosha. Serikali imetoa Shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya kununulia mbegu za mazao ya muda mfupi na yanayokomaa haraka katika Mikoa iliyoathirika na ukame. Napenda nitumie fursa hii kusisitiza umuhimu wa Wakuu wa Mikoa na Wilaya kusimamia upatikanaji na usambazaji wa mbegu hizo ili wakulima waweze kutumia mvua hizi vizuri. Ni vyema viongozi wote wakiwemo Waheshimiwa Wabunge, Madiwani, tushirikiane kwa karibu kuhakikisha utekelezaji wa zoezi hili unakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ukame uliotukumba umetukumbusha usahihi wa Ilani ya Uchaguzi wa CCM kuhusu kilimo. Ili kuepukana na madhara ya uhaba wa chakula, tunapaswa kufanya mapinduzi katika kilimo. Ilani ya CCM ya mwaka 2005 inatuasa na mimi nanukuu: “Mapinduzi katika kilimo ni changamoto kubwa katika mchakato wa kujenga uchumi wa kisasa kwa sababu kubwa tatu. Kwanza, Mapinduzi ya Kilimo yanaongeza sana ufanisi na tija katika uzalishaji na hivyo kuongeza mavuno kwa wingi.

Pili, mazao ya kilimo ni mazao ya biashara. Kwa hiyo, ongezeko la mavuno linawezesha wakulima kufaidika kutokana na kuuza ziada kubwa zaidi kwenye soko na nchi inafaidika kwa kuuza mazao mengi zaidi nchi za nje.

Tatu, Mapinduzi katika kilimo yanaunda mazingira muafaka kwa ujio wa mapinduzi ya viwanda kwa vile hali hii itavutia uanzishaji wa viwanda vya usindikaji na utengenezaji wa bidhaa za viwandani kutokana na mazao ya kilimo. Kilimo cha kisasa ndiyo msingi wa uchumi wa kisasa.” Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kilimo ndio mhimili wa uchumi wa nchi yetu, kwani kinachangia kati ya asilimia 45-50 ya pato la Taifa letu. Hata hivyo, kilimo chetu bado ni duni sana na chenye eneo dogo linalolimwa. Tanzania ina jumla ya hekta milioni 94 zinazofaa kwa kilimo na mifugo ambazo kati yake hekta milioni 50 zinafaa kwa mifugo na hekta milioni 44 zinazofaa kwa kilimo. Lakini hekta milioni 10.1, sawa na asilimia 23 tu ndizo zinazotumika kwa kilimo hivi sasa.

Aidha, kutokana na kilimo duni, uzalishaji wa mazao kwa hekta ni kidogo sana. Kwa mfano, wakulima wa pamba huzalisha kati ya kilo 300 hadi 450 kwa hekta wakati vituo vya utafiti vinaonesha uwezo wa kuzalisha kilo 1,500 hadi 2000 kwa hekta. Hii ina maana kuwa mkulima mwenye hekta 2 atavuna kati ya kilo 600 hadi 900 wakati angeweza kuvuna kati ya kilo 3,000 hadi 4,000 katika hekta hizo mbili.

Mheshimiwa Spika, wakulima wa mahindi katika Nyanda za Juu Kusini wasiotumia mbolea na mbegu bora hupata wastani wa magunia 20, kwa hekta. Kwa upande mwingine wakulima wanaotumia mbolea na mbegu bora na kufuata kanuni za kilimo cha kisasa, hupata wastani wa magunia 70. Kwa hiyo, wakulima wasiotumia pembejeo na kutokufuata kanuni za kilimo bora, hupoteza fursa ya kupata maguni 50 ya mahindi. Changamoto kubwa iliyoko mbele yetu ni ya kuwasaidia wakulima kupata na kufuata mbinu na kanuni bora za kilimo cha kisasa na pembejeo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 1972 Chama cha *TANU* wakati huo kilitoa tamko la Iringa kuhusu kilimo lililoitwa: "Siasa ni Kilimo." Tamko lile lilisisitiza umuhimu wa kuwafikishia wakulima utaalamu wa kilimo. Ni takriban miaka 34 tangu tamko hilo litolewe. Tujiulize, hivi wataalam wetu wameweza kuleta mabadiliko ya kilimo cha wakulima wetu?! Tangu wakati huo wameleta mageuzi gani katika uzalishaji wa mazao ya kilimo? Hivi wapo wanaowasimamia na kukagua kazi wanazofanya Maafisa Ugani wa Kilimo walioko Vijijini? Kuna tatizo gani la kitaalam? Mbona tunao wataalam wengi wazuri kwenye kilimo? Chuo Kikuu cha Kilimo tunacho ambacho kinatoa wataalam wengi kila mwaka.

Aidha, kwa miaka kadhaa tumekuwa tukielekeza asilimia kubwa ya bajeti ya Serikali katika kilimo. Tatizo ni nini? Labda tujiulize ni lini wataalam wetu watatufikisha katika kuleta mageuzi katika kilimo? Wakati umefika kwa wataalam wetu kuleta mageuzi ya msingi katika kilimo. Wizara zinazohusika, Uongozi wa Mikoa, Wilaya kwa kushirikiana na Wataalam waliopo lazima watafute mbinu mpya za kuleta mageuzi katika kilimo. Lazima kuwepo na ufuatiliaji wa karibu wa shughuli wazifanyazo Wataalam wa Kilimo. Lazima kuwepo na uwajibikaji kwa wahusika katika ngazi zote. Mahali alipo Mtaalam wa Kilimo kazi zake zilizomo katika mpango, kazi zipimwe kwa kulinganisha na mafanikio ya kilimo katika eneo analolihudumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kilimo cha umwagiliaji kina uwezo mkubwa wa kutuwezesha kuongeza tija katika kilimo. Nchi zinazoendelea ambazo zimekipa kipaumbele kilimo cha umwagiliaji zimefanikiwa sana. Tunayo mifano ya nchi za India, Pakistan, China na Misri na kadhalika. Nchi hizo zimeweza kuzalisha chakula kwa wingi cha kutosheleza mahitaji ya ndani na ziada kuuza nje.

Mpango Kabambe wa Umwagiliaji Maji unaonesha kuwa Tanzania ina jumla ya hekta milioni 29.4 ambazo zinafaa kwa kilimo cha umwagiliaji. Licha ya ukubwa huo wa eneo linalofaa kwa umwagiliaji ni hekta milioni 0.25 (hekta 250,000) tu ndizo zimeendelezwa. Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete, katika Hotuba aliyoitoa Bungeni tarehe 30 Desemba, mwaka jana 2005 alisisitiza na nanukuu: "Serikali itahakikisha kuwa Mpango Kabambe wa Umwagiliaji Maji unaongezewa fedha na Wataalam ili tupanue maeneo yanayotumika hivi sasa kwa kilimo cha umwagiliaji maji.

Vile vile, tutahakikisha kuwa utaalam wa asili wa kilimo cha umwagiliaji unafufuliwa, pamoja na miundombinu yake." Mwisho wa kunukuu. Wakati umefika wa kutumia fursa hii kubwa kuendeleza kilimo cha umwagiliaji nchini. Ili kutekeleza azma

hii, lazima tujiwekee malengo ya kuridhisha ya kuendeleza kilimo cha umwagiliaji kwa kila mwaka ili kuondokana na aibu ya kuomba chakula kila wakati ukame unapoikumba nchi yetu. Viongozi katika ngazi zote za utekelezaji tuwajibike katika kusimamia kwa uadilifu miradi ya umwagiliaji maji mashambani. Kama alivyoelekeza Mheshimiwa Rais. Bajeti kubwa ya Serikali mwaka huu itaelekezwa katika kuendeleza kilimo, ufugaji na uvuvi. Tunaomba Waheshimiwa Wabunge mtuunge mkono katika hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mifugo hatujaweza kutumia kikamilifu mifugo tuliyonayo. Ilani ya CCM ya Uchaguzi ya mwaka 2005 inaainisha maeneo ambayo tunaweza kuyaboresha ili kuongeza tija katika Sekta ya Mifugo. Maeneo hayo ni ujenzi wa mabwawa na majosho, elimu kwa wafugaji ili waweze kutekeleza kanuni bora za ufugaji na maeneo ya kuzuia uharibifu wa mazingira unaotokana na mifugo. Maeneo mengine ni yale yanayohusiana na uboreshaji wa malisho ya mifugo na kupunguza migogoro ya wakulima na wafugaji kwa kutenga maeneo maalum ya kulisha mifugo. Kwa kutumia mwongozo wa Ilani ya CCM, kilichobaki ni utekelezaji ambao kila mmoja wetu anahitaji kuwajibika katika nafasi yake.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Uvuvi nayo ina nafasi kubwa ya kuchangia katika ukuaji wa uchumi na hali bora ya maisha ya wananchi wetu. Ipo fursa kubwa ya kupata lishe bora kutokana na uvuvi, kuongeza kipato, ajira, mauzo nje na kuboresha hali ya maisha ya wavuvi na wananchi. Tena Ilani ya Uchaguzi ya CCM imetuhimiza kuwekeza katika kutumia maliasili zilizomo katika bahari, maziwa na mito ili wavuvi watumie fursa zake kuinua hali zao za maisha. Kwa mtazamo huu wadau wote wa Sekta ya Uvuvi hatuna budi kuisaidia sekta hii ikue kwa haraka zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali inao utaalam mkubwa wa kuandaa sera nzuri, mikakati na mipango mizuri inayokubalika hata na marafiki zetu wa maendeleo. Lakini tatizo letu ni la uwajibikaji hafifu kwa Viongozi na Watendaji katika kutekeleza malengo yanayoainishwa katika sera na mipango hiyo. Hatuna budi kujisahihisha na kutimiza wajibu wa kila mmoja wetu. Bila uwajibikaji katika kusimamia utekelezaji wa malengo ya mipango yetu, hatuwezi kwenda na ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete katika Hotuba aliyoitoa Bungeni tarehe 30 Desemba, 2005 alieleza kuhusu utendaji Serikalini kama ifuatavyo:

"Tutahimiza utekelezaji wa majukumu ya Serikali kwa ustadi, kwa uharaka na kwa ufanisi. Tunataka Watendaji wa Serikali wenye uadilifu wa hali ya juu na wenye kuzingatia misingi ya uwajibikaji." Mwisho wa kunukuu.

Tunachohitaji ni kubadilika na kwenda kwa kasi mpya na uwajibikaji. Kuanzia sasa viongozi katika ngazi zote kitaifa hadi Vijijini wasimamie na kuhakiki utekelezaji wa malengo ya walio chini yao tutakapotembelea Mikoa tupate taarifa na kuona hatua madhubuti za Mikoa za kuibua miradi ya maendeleo na kuisimamia kikamilifu. Watendaji wote watapimwa kwa vigezo vya jinsi wanavyochangia katika maendeleo ya shughuli za kiuchumi za wananchi na zile za huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nia ya kutekeleza azma yake ya kuongeza ufanisi katika utendaji kazi Serikalini, Serikali iliamua kuwafanya Maafisa Wakuu Serikalini kuingia Mikataba na Serikali katika kutekeleza majukumu waliyopewa, yaani *Performance Agreements*. Utaratibu huu huwataka Wakuu wa Idara kuingia Mikataba na Makatibu Wakuu wao inayoonyesha kazi wanazotaka kuzitekeleza ili malengo yaliyopangwa yafikiwe na Wizara hiyo katika kipindi cha mwaka wa fedha unaohusika, kutumia fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa Wizara hiyo katika kipindi hicho. Vivyo hivyo Wakuu wa Idara nao huingia Mikataba ya aina hiyo hiyo na Maafisa Waandamizi katika Idara zao.

Lengo la kuwa na *Perfomance Agreements* ni kuweka vipimo vya utendaji kazi kwa gharama zinazokubalika katika kipindi kinachojulikana. Hii ni kuiwezesha Serikali kutathmini utendaji kati wa wafanyakazi wake katika ngazi zote na hivyo kuwajua wanaotekeleza wajibu wao ipasavyo na kuwatunuku na kuwachukulia hatua za kinidhamu na kisheria wale ambao watashindwa kutekeleza kazi walizopewa. Wale ambao wataonekana hawafai kabisa kuwa kazini Serikali inakuwa na sababu za wazi za kuwaondoa.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu umekwishaanza kutumika kwenye Mashirika ya Umma kwa mfano Wizara ya Maji tayari ina Mikataba na mamlaka za Maji Mijini, yaani *Urban Water and Sewarage Authorities* jambo ambalo linaiwezesha Wizara hiyo kupima utendaji wa mamlaka hizo kila mwaka na kujua matatizo yanayokabili utendaji kazi wa mamlaka hizo na kutafuta njia ya kukabiliana na matatizo hayo.

Tathmini ya utekelezaji wa kazi chini ya Mikataba hiyo inaiwezesha Serikali kujua ubovu uko wapi na kufanya marekebisho pale inapoonekana kwamba Menejimenti ndiyo imeshindwa kutekeleza wajibu wake bila sababu za msingi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Serikali inakusudia kuanzisha utaratibu huu wa *Perfomance Agreements* kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa. Lengo ni kuzifanya Halmashauri za Wilaya zitekeleze wajibu wake ipasavyo kwa kuweka malengo fasaha ya maendeleo katika Sekta zote ili kuinua maendeleo ya wananchi wao na uchumi wa nchi yetu kwa ujumla. *(Makofi)*

Mikataba hiyo inaandaliwa na itakuwa tayari kuwekwa saini kati ya Serikali na Halmashauri za Wilaya zote za Tanzania Bara kuanzia Julai, 2006. Mikataba hiyo itasisitiza umuhimu wa kuwa na mipango makini yenye matokeo yanayoonekana kwa kutumia fedha kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato ya Halmashauri, michango ya wananchi wenyewe, wafadhili mbalimbali na fedha kutoka bajeti ya Serikali Kuu zitakazoidhinishwa kwenye Bajeti za Halmashauri.

Tathmini ya utekelezaji wa Mikataba hiyo ya utendaji kazi kwenye Halmashauri za Wilaya na Serikali za Mitaa itaiwezesha Serikali Kuu kujua ni wakina nani wanahujumu nguvu za wananchi na za Serikali kwa manufaa yao wenyewe. Kwa hiyo, nazielekeza Halmashauri zote nchini zijiandae ipasavyo kuingia kwenye Mikataba hiyo na Serikali Kuu. Ni vyema niseme toka mapema kwamba Serikali haitawavumilia

Watendaji katika ngazi zote watakaodhihirika kuwa wahujumu na wala jasho la wataka maendeleo na itawachukulia hatua kali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge watakumbuka kwamba tarehe 17 Machi mwaka huu 2006 majira ya saa 10 jioni jengo la ghorofa tano lililokuwa likijengwa katika eneo la Keko Machungwa pale Dar es Salaam liliporomoka na kusababisha kifo cha mtu mmoja. Kutokana na tukio hilo Serikali ilichukua hatua zifuatazo:-

(a) Kuanza uchunguzi wa kina kuhusiana na ajali hiyo;

(b) Kusimamishwa kazi kwa Mhandisi wa Manispaa ya Temeke; na

(c) Kuwachukulia hatua za kisheria wahusika wote pamoja na mmiliki wa jengo la *Chang'ombe Village Hotel.*

Mheshimiwa Spika, ingawa tukio hilo limetokea Dar es Salaam kwenye eneo ambalo sio la kibiashara huenda likawa ni kielelezo cha kuwepo kwa tatizo kubwa zaidi katika maeneo mengine nchini, hivyo kama hatutachukua hatua za kudhibiti ujenzi holela katika Miji, majanga makubwa zaidi yenye kuathiri maisha na mali za watu yanaweza kutokea.

Kadhalika, tukio hili linaweza kutumika kama kiashiria cha umuhimu wa Serikali kutathmini upya tatizo sugu la ujenzi holela na hasa katika maeneo yaliyopimwa Mijini hususani katika Jiji la Dar es Salaam maeneo ya Kariakoo. Kwa mfano iko haja ya kuangalia kama wamiliki wa majengo mengi yaliyopo Kariakoo wametimiza masharti ya ujenzi. Na ni kwa kiasi gani, kwa mfano maghorofa yaliyopo Kariakoo yamezingatia ujazo wa kiwanja, ukubwa na mpangilio wa vyumba, uimara wa jengo, kuwepo kwa mifereji ya majitaka na kadhalika. Serikali imeamua kuunda Kamati Maalum ya Kitaifa ambayo itakagua ujenzi Jijini Dar es Salaam na hasa Kariakoo ili kujiridhisha na uimara na usalama wa maghorofa hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Halmashauri za Miji, Manispaa na Jiji ipo tabia ambayo imeanza kujitokeza ya baadhi ya watu ama kwa makusudi au kwa kutojua Sheria wameamua kufanya yafuatayo:-

(a) Kujenga bila kibali cha ujenzi;

(b) Kujenga bila kuzingatia michoro iliyobuniwa;

(c) Kuingia katika maeneo ya matumizi mengine kama vile barabara, Shule, makaburi na maeneo ya wazi;

(d) Kujenga vituo vya mafuta kwenye maeneo ya makazi; na

(e) Kujenga majengo zaidi ya moja kwenye kiwanja kimoja na pale wanapopelekwa Mahakamani kufanya mbinu za hila kuchelewesha na kushinda kesi hizo. Kutokana na hali hiyo, Serikali inakusudia kusimamia kwa karibu zaidi Sheria, Kanuni na Taratibu za Mipango Miji na Ujenzi Mijini. Kwa maana hiyo, Serikali imeamua kuunda Kamati Maalum katika kila Halmashauri za Miji ambazo zitakuwa na jukumu la kukagua majengo yote yaliyojengwa na yanayojengwa katika Halmashauri hizo. Katika ukaguzi huo, Kamati zinatakiwa kubaini na kujiridhisha kama taratibu zote za ujenzi wa majengo zimezingatiwa.

Mamlaka zinazohusika zinatakiwa kupitia taarifa za Kamati hizo na kuchukua hatua zinazopasa. Serikali pia imeamua kufuatilia kwa karibu kesi zote za muda mrefu zinazohusu masusla ya ardhi ambazo zipo Mahakamani kwa nia ya kuhakikisha kwamba zinamalizika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uwezo wa Serikali kutoa huduma mbalimbali kwa wananchi unategemea wingi wa mapato yanayoweza kukusanywa kulingana na mipango iliyowekwa. Matukio ya dharura na yasiyotabirika ni vikwazo vikubwa katika mipango na bajeti ya Serikali. Hivi karibuni kutokana na majanga ya njaa, mlipuko wa viwavijeshi na upungufu wa umeme, Serikali imelazimika kutumia kiasi cha fedha za bajeti kama alivyoeleza Mheshimiwa Rais kwa ajili ya kununua chakula na mbegu pamoja na kuzisambaza na kuboresha mitambo ya umeme.

Wakati huo huo, majanga hayo yameathiri pamoja na mambo mengine vyanzo muhimu vya upatikanaji wa mapato ya Serikali. Kutokana na hali hiyo, Serikali imedhamiria kuimarisha usimamizi katika ukusanyaji wa mapato yake ili kuhakikisha kuwa mapato yote yaliyokusudiwa katika bajeti ya 2005/2006 yanapatikana. Aidha, tutalazimika kuchukua hatua muhimu kuziba mianya ya ukwepaji kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa baadhi ya hatua zitakuwa na gharama pengine za muda mfupi lakini ni lazima kuzichukua ili kuongeza mapato ya Serikali. Eneo tunalolitazama kwa sasa ni mapato ya kodi yatokanayo na mafuta ya *diesel* na *petrol*. Serikali imetoa maagizo kwa *TRA* kuimarisha ukusanyaji wa mapato yote ya Serikali na kuziba mianya ya ukwepaji kodi hasa katika eneo la mafuta ya *diesel* na *petrol.* Katika hatua za awali, Serikali imeziagiza mamlaka zinazohusika ikiwemo Mamlaka ya Bandari ziharakishe ufungaji wa *flow metres* katika Bandari ya Tanga ili kuziba mianya yote ya ukwepaji kodi ambayo imeanza kujitokeza baada ya *flow metres* kufungwa katika Bandari ya Dar es Salaam.

Eneo lingine ambalo ni lazima tulidhibiti ni uingizaji wa mafuta na bidhaa nyinginezo katika eneo la Ziwa Victoria. Lengo letu ni kuhakikisha kuwa kila senti ya kodi iliyopangwa kukusanywa inapatikana. Viongozi na Watendaji watakaokuwa kiwazo katika kuiwezesha Serikali kupata mapato yake itabidi wachukuliwe hatua kali na za kinidhamu. Hatua za aina hiyo zimeanza kuchukuliwa na zitaendelea. Ni wajibu wa Serikali kukusanya kodi na haitaruhusu hata kidogo baadhi ya watu kutumia uwezo wao wa fedha na nafasi zao katika jamii za utendaji ama za uongozi Serikalini kutukwamisha. *(Makofi)*

Lakini tunawaomba pia wananchi wawe walinzi wa maeneo yao kwa mfano, kama unajua na una ushahidi kwamba mshindani wako kibiashara katika eneo fulani anakwepa kodi ya Serikali, iarifu mamlaka inayohusika ili wachukue hatua hii. Ndiyo maana ya kuwa na uwanja sawa wa kibiashara, yaani *Level Playing Field.*

Mheshimiwa Spika, napenda nimalizie kwa kukumbusha na kusisitiza machache yafuatayo:-

(a) Mvua zinanyesha. Tuelekeze nguvu zetu sasa katika kilimo cha mazao ya muda mfupi na yanayokomaa haraka;

(b) Tuhimize kilimo cha umwagiliaji na tuwahimize wananchi wetu kupanua mashamba yao maradufu ili kuongeza mazao zaidi. Aidha, tutumie matumizi ya Pembejeo na kanuni za kilimo bora;

(c) Tuendelee kuhimiza wananchi kujitolea kujenga Shule za Sekondari ili ifikapo Januari, 2008 kilele cha matokeo ya Mradi wa MEM wanafunzi wengi zaidi wapate nafasi ya kusoma Sekondari. Ujenzi wa madarasa uende sambamba na ujenzi wa nyumba za Walimu, Maabara na vyoo vya kutosha. Aidha, Wizara nazo zisimamie kwa haraka upatikanaji wa Walimu;

(d) Wananchi wahimizwe kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za Mipango Miji katika ujenzi wa majengo Mijini; na

(e) Usimamizi wa ukusanyaji mapato ya Serikali uimarishwe katika ngazi zote za Serikali kuu na Halmashauri za Mitaa. Mianya ya upokeaji rushwa idhibitiwe na ile ya ukwepaji kodi.

Mheshimiwa Spika, napenda kumalizia kwa kuwashukuru wote waliosaidia kufanikisha Mkutano huu. Shukrani za pekee ni kwako wewe Mheshimiwa Spika, kwa kuendelea kutuongoza kwa kasi mpya, ari mpya, nguvu mpya na kwa viwango vinavyopasa. Nampongeza pia Mheshimiwa Naibu Naibu Spika, Anne Makinda, kwa kutuongoza vizuri.

Nawashukuru vilevile Wenyeviti wa Bunge, Mheshimiwa Jenista Mhagama - Mbunge wa Peramiho na Mheshimiwa Job Ndugai - Mbunge wa Kongwa, kwa msaada mkubwa waliokupa katika kuliongoza Bunge letu. Aidha, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yenu mbalimbali wakati wa kujadili Miswada tuliyoipitisha katika Mkutano huu.

Namshukuru Katibu wa Bunge na Wasaidizi wake pamoja na Wataalam wote wa Serikali kwa misaada yao ya kitaalam na ya huduma mbalimbali iliyofanikisha kikao chetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nawatakia wote safari njema na sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu, liahirishwe sasa hadi siku ya Jumanne, tarehe 13 Juni, 2006 saa tatu asubuhi, litakapokutana hapa Mjini Dodoma, kwenye Ukumbi mpya wa Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijawahoji kuhusu hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kuliahirisha Bunge hili, mnivumilie nina maneno machache sana ya shukrani kama ifuatavyo:-

Kwanza nimshukuru yeye mwenyewe Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri ambayo imejaa maneno ya hatua za utendaji. Hicho ndicho mimi nimekiona. Hotuba hii siyo shairi, hotuba hii ina mambo ya utendaji na hii inatuelekeza pazuri kwa sababu hivyo ndiyo inatakiwa iwe Serikali inayotenda mambo iliyoahidi.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahsante sana. *(Makofi)*

Napenda niwashukuru Waheshimiwa Mawaziri wote na Manaibu Waziri kwa jinsi ambavyo wamekidhi viwango vya kujibu maswali na kujibu hoja katika Ukumbi huu. Nina hakika Waheshimiwa Wabunge mtakubaliana nami kwamba Bunge hili limepata bahati ya kuwa na Baraza ambalo kwa kweli linajituma.

Nilipotoa rai siku mmenichagua kwamba tutafurahi Serikali yetu iwe makini, nadhani wengi wenu hata ukiwasikiliza wananchi huko nje wanaona kwamba mwanzo huu ni mzuri. Sasa naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu msilegeze kamba. *(Makofi)*

Naomba niwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kunivumilia, mara kadhaa nimejikwaa, lakini kama mnavyofahamu, hakuna Shule ya Ubunge wala Uspika. Naomba mwendelee kuniunga mkono, kunisaidia, kunipa ushirikiano kwa sababu ninayo dira ya kushirikiana nanyi kulifanya Bunge la Tanzania ndani ya miaka mitano liwe ni Bunge bora kuliko yote katika Afrika. *(Kicheko/Makofi)*

Wale ambao mnafuatilia katika Vyombo vya Habari, mtaona tangazo la Ofisi ya Bunge la kuita Wataalam wa Kimataifa na wa ndani wa kututengenezea mpango wa maendeleo wa miaka mitano wa Bunge hili. Zabuni zimekwishaitishwa na zitatusaidia sasa kutengeneza mipango ya mwaka hadi mwaka ya kuliimarisha Bunge kwa kila hali. *(Makofi)*

Pia niseme tu kwamba Serikali yoyote makini haiogopi Bunge lililo makini. Kwa hiyo, nakuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu mtusaidie pale tunapohitaji nyenzo za kuliimarisha Bunge, basi msisite na Waheshimiwa Wabunge tuendelee kuwasaidia wananchi kuelewa kwamba Bunge lililo imara, Bunge lililowezeshwa ni nyenzo muhimu sana ya maendeleo ya nchi. *(Makofi)*

Mimi naamini kabisa kwamba mengi tutayaweza na yale ya awali ambayo nimekwishayafikisha Serikalini kwa niaba yenu, ya kuliimarisha Bunge, nina hakika tutapata majibu ndani ya muda usio mrefu sana. *(Makofi)*

Sasa nimalizie tu kwa kuwashukuru Watumishi wa Bunge. Ndugu zangu Wabunge, kwa kweli mimi nimeshangazwa sana! Vijana hawa wanafanya kazi kubwa sana! Tuna hazina nzuri sana ambayo inastahili tuilee vizuri. Naelewa maslahi ya Watumishi wa Bunge hivi sasa yako chini sana ya kiwango. Sasa, leo wenzangu wa Tume ya Huduma tunaianza kazi ya kuweza kuona pale kulingana na hali ya uchumi wetu tunaweza kufanya nini kuwasaidia vijana hawa ili wazidi kutuhudumia kwa vizuri zaidi. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo, sasa nitawahoji kuhusu hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ya Kuahirisha Bunge.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Pamoja na Waheshimiwa kadhaa kutaka kubakibaki Dodoma, ukitaka kubaki Dodoma wewe huhitaji ridhaa ya Spika. *(Makofi)*

*(Saa 11.47 asubuhi Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumanne,*
*tarehe 13 Juni, 2006 saa tatu asubuhi)*